Kuacha Yote

Ketini. Nilitaka kusema habari za jioni kwa wote. Nina furaha sana kuwa hapa usiku wa leo. Nayahesabu tu haya kuwa ni majaliwa mazuri sana kuwa hapa, kanisa hili jipya linalopendeza, kumwabudu Bwana. Tumekuwa tukitarajia hili, kuja huku, kwa muda fulani, kwa ajili ya wakati wa ushirika pamoja na watu, na kuzifurahia baraka, na kutumaini kwamba tutakuwa baraka kwenu enyi watu. Basi wakati juma limeanza kuendelea sasa, na hapo tunajua ule mkutano mkubwa unakuja sasa, kuanzia Alhamisi.

2 Nami ndio kwanza nisikie alasiri ya leo, kwa Ndugu Williams, ya kwamba tuna mshangao mzuri wa Alhamisi usiku. Ndugu Oral Roberts atakuwa pamoja nasi, kuzungumza, Jumatano usiku. Huo bila shaka utakuwa ni mshangao mzuri kwetu sisi sote, kwa kuwa Ndugu Oral bila shaka ni msemaji hodari. Na litakuwa ni jambo zuri kupata kumwona, mimi mwenyewe, tena, kumsalimia kwa mkono.

3 Nasi tulikuwa huko Tempe jana usiku, kwenye Assembly of God, ninaamini ilikuwa, huko juu. Na—na bila shaka tulikuwa na wakati mzuri sana jana usiku huko Tempe. Nasi tumekuwa na wakati mzuri katika kila kanisa ambalo tumekuwa tukitembelea hapa kwenye eneo la Phoenix, na pia huko juu Tempe. Nasi tunathamini tu mambo haya sana, hata ni vigumu kwetu kuyaeleza.

4 Ni kwa nadra sana ninapata nafasi ya kufanya jambo hili, kuja tu usiku mmoja katika kila kanisa, na kuzungumza na watu na ndugu wahudumu. Nayo inanipa nafasi kidogo ya kuonyesha shukrani zangu juu ya watu hawa, madhehebu haya mbalimbali na makundi ya watu. Kwa sababu, ni, hao ni wadhamini wakubwa hudumani, katika huduma za nchi za kigeni na kila mahali, na kwa njia hii kidogo ninaweza kupata nafasi kidogo ya kuonyesha jinsi ninavyojisikia kuwahusu, katika kuonyesha shukrani.

5 Nasi tumekuwa na walio huru na ninii . . . ninaamini, Church of God, Assemblies, na kila moja; na, katika nchi za ng'ambo, Foursquare, Church of God, Assembly of God, na Jina la Yesu. Nayo, yote hayo, yote yanaonekana tu ni moja tunapokutanika pamoja kufanya mkutano kule kwenye viwanja vya vita. Basi, mwajua, hapa nyumbani huenda kukawa na mawazo kwamba huenda tukatofautiana, bali inapofikia kwenye uwanja wa vita, mbona, hakuna tofauti wakati huo. Mnaona?

6 Nililelewa katika familia kubwa. Kulikuwako na watoto kumi. Nasi wavulana tungeenda kwenye baraza la nyuma, nasi tungepigana mmoja na mwenzake, loo, jamani. Wavulana

tisa, msichana mmoja, nasi kweli tungepigana. Lakini mtu asithubutu kumchokoza mmoja wetu, huko kwenye baraza la mbele, maana, wakimchokoza mmoja, walivamiwa na wa Branham kutoka kila mahali. Kwa hiyo nafikiri hivyo ndivyo ilivyo na watoto wa Mungu, Kanisa.

7 Hapa miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa huko Houston, nasi tulikuwa na mkutano mkubwa. Na huko pamoja na... Nilikuwa na wadhamini kadhaa kule; Ndugu Raymond Richey, na—na Assemblies of God, na—na watu wa Jina la Yesu, na wote wengine mbalimbali. Nasi tulikuwa na mkutano mkubwa. Nasi tulikuwa kwenye Jumba la Muziki. Vema, tungewaketisha yapata elfu nane, nadhani.

8 Nako kulikuwa na m—mhudumu wa Kibaptisti aliyetaka kunipa changamoto katika majadiliano, juu ya Biblia, kwamba uponyaji wa Kiungu haukuwa sahihi. Vema, nimepitia mengi sana ya hayo. Kwa nini kupoteza usiku juu ya mtu mmoja asiyeamini, wakati kuna maelfu wameketi pale wapate kuombewa, mnaona? Kwa hiyo basi yeye akaliweka kwenye gazeti, kwamba niliogopa kufanya hivyo.

9 Ndipo mzee Ndugu Bosworth, yule mwenye karibu umri wa miaka themanini, yeye alisema, "Loo, hebu nifanye hivyo."

10 Nami nikawazia juu ya Kalebu, mwajua, "Hebu nichukue mlima huu." Kwa hiyo nikasema, "Ndugu Bosworth, ni—nisingekutaka uzozane. Kristo hataki sisi Wakristo tuzozane. Kama mtu huyo ni asiyeamini, mbona, yeye ni asiyeamini tu, hivyo tu. Hakuna kitu unachoweza kufanya juu yake."

11 Na kwa hiyo akasema, "Vema, jambo ni kwamba," kasema, "kama tukiondoka, wakiisha kuandika hilo gazetini," kasema, "watasema ya kwamba sisi ni kundi tu la, mwajua, hatujui tunalozungumzia, mhemko tu wa kujichochea." Akasema, "Laiti ungalinipa hiyo nafasi." Ndipo nikamwangalia amesimama pale, karibu umri wa miaka themanini, na mwenye matumaini vivyo hivyo katika Maandiko hayo.

12 Nikasema, "Vema, Ndugu Bosworth, kama utanipa mkono na kuahidi hutazozana."

13 Akasema, "Loo, sitazozana." Kwa hiyo huyo akashuka chini, akamwambie huyo mwandishi wa habari.

14 Hakika, mnajua jinsi magazeti yanavyoweza kuirusha, mnaona. "Manyoya ya kikanisa yatapeperuka," mwajua.

15 Tukaupata uwanja wa michezo, uwanja wa mbio, ndipo usiku huo tulikuwa na yapata watu elfu thelathini huko nje. Ndipo basi ikaonyesha pale, ya kwamba watu walikuja kwa ndege, magarimoshi. Nawaambia, walikuwa wakipanda ngamia wa nundu moja, ngamia wa nundu mbili, na ngamia wa nundu tatu, lakini wote walikuwa wakikinywea kisima kile ambamo mna nafasi kwa ajili ya sisi sote, vivyo hivyo. Kila kitu kilikuwa

pamoja. Nayo inaenda . . . Nilipata tu baraka kuu kutokana na hilo, kuwazia sasa. Mnaona, wakati kweli magumu yanapokuja, kulikuwa na kitu kimoja tulichokuwa nacho shirika, sote tuliamini katika Roho Mtakatifu na uponyaji wa Kiungu. Kwa hiyo kila mtu akaja kuchangia sehemu yake.

16 Na kwa hiyo tunajua yaliyotukia usiku huo, jinsi ambavyo Roho Mtakatifu alichukua mamlaka. Basi hapo ni wakati Malaika wa Bwana aliposhuka. Walimpiga picha. Kisha—kisha ikatoka huko ikaenda Washington, DC, kwa ajili ya kuthibitishwa. Kisha, baada ya hapo, ilichukuliwa na uchunguzi na kadhalika. Naye George J. Lacy, mkubwa wa FBI, aliiandika ile—ile hati juu yake. Naye ndiye mkubwa wa hati za alama za vidole za—za FBI. "Ilikuwa ni Kiumbe cha kimbinguni kabisa. Nuru hiyo iligusa lenzi. Haikuwa saikolojia." Akasema, "Mara nyingi nimesema mikutano yako ilikuwa ni saikolojia, pia. Nilidhani ulikuwa ukizisoma akili za watu hao." Akasema, "Lakini jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia, Bw. Branham. Iligusa hiyo lenzi." Akasema, "Iko hapa."

17 Kwa hiyo, basi, Hiyo imepigwa picha. Ilipigwa picha kabla ya hapo, na mara kadhaa baada ya hapo. Ninii tu, nina shukrani sana kujua. Watu wengi hapa wameiona picha hiyo, sivyo? Nadhani, loo, wengi wenu mnayo.

18 Nina furaha sana kujua hilo hata ingawa huduma ya Kipentekoste katika siku hizi za mwisho imezungumziwa, bali, nawaambieni, katika kuichukua historia ya Biblia . . .

19 Ndio kwanza nipitie hi—historia ya kanisa, miaka kadhaa iliyopita, kutoka kwenye kifo cha mtume wa mwisho, Yohana, kwenye kisiwa cha . . . hapo alipoondoka kwenye Kisiwa cha Patimo, naye akaingia na—na akamaliza kuviandika Vitabu na kuviweka pamoja. Yeye aliwekwa huko nje kwa sababu alikuwa akiyachukua Maandishi ya mitume na kufanya Biblia kutoka Kwake. Na hiyo ndiyo sababu alipelekwa kwenye Kisiwa cha Patimo. Akiisha kuchemshwa kwenye grisi usiku na mchana, kisha kumweka huko nje kisiwani. Naye akavikusanya hivyo Vitabu pamoja. Na isitoshe, Mungu akampa kile Kitabu cha mwisho cha Biblia, Ufunuo.

20 Ndipo basi kurudi, nikaanza kwenye historia yake pale, halafu kwenye ninii yake . . . mmoja wa wafuasi wake, Polikapu, Ignatius, na wengi wao, na kuendelea mpaka kwa Martin, Ireneo, Justus, Mtakatifu Columba, na kote kote, kushuka kwenye ule wakati wa giza, na kote kote, mpaka kwa Lu—Lutheri, na Wesley.

21 Nami nimekuja kuona kwamba, hata tangu siku za mitume, katika huo utendaji kazi mkubwa wote wa Roho Mtakatifu, hakuna mmoja wao unaozidi mwenendo huu wa mwisho wa Bwana, hapa katika siku hizi za mwisho. Hatuyatambui hayo,

enyi marafiki. Yapo mambo yanayotukia sasa ambayo yanaweza kumthibitisha Mungu, kama ile picha ya—ya Kristo, moja kwa moja pamoja nasi, ambayo hawakuwa na mitambo ya kuyafanya nayo, katika siku hizo. Lakini sasa mwanadamu anajaribu kufanikisha jambo fulani, kuondoa kutoka kwa Mungu, naye Mungu huchukua ufanisi uo huo na kujithibitisha Mwenyewe nao. Kwa hiyo ni ninii tu . . . Kamwe hutaweza kumtangulia Mungu, maana Yeye yuna nguvu zote, anaenea kila mahali, hana kikomo. Hakuna njia ya kuliondokea. Inatupasa tu kuwa wanyenyekevu na kumtumikia Yeye, ndilo jambo bora kuliko yote nijualo kufanya.

22 Ninaona aibu, bali siamini ninajua jina la mchungaji, hapa kanisani. Mimi . . . [Ndugu Griffith analitaja jina lake—Mh.] Ndugu Griffith, bila shaka nina furaha kukutana nawe, ndugu, na wakati wa kuja hapa na ushirika huu, kuwa pamoja nanyi, kuninii . . .

23 Sikuzote tunapenda kulizungumzia namna hii, kwa wale wanaokaa kwenye Sunnyslopes, kwa sababu sisi ni wasafiri hapa, wageni. Tunakiri ya kwamba haya si makazi yetu. Sisi ni uzao wa Ibrahimu, "Tukiutafuta Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu."

24 Hii ni nchi ya kupendeza. Sifikiri kuna kitu mfano wake, nilichopata kukiona. Nami husafiri karibu kila taifa ulimwenguni, wala sijapata kuona chochote huko Uropa, Italia, Asia, popote katika Mashariki, ambacho kalilingana kamwe na Phoenix, Arizona. Sasa, hiyo ni kweli. Ndipo mahali pazuri sana nilipopata kupaona. Lakini, loo, utaonekana kama kichochoro, ukilinganishwa na jinsi itakavyokuwa kwenye ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Kwa hiyo tuna—tuna . . .

25 Haya siyo makazi yetu. Sisi ni wasafiri tu hapa, nasi tumekuja kufanya ushirika huu pamoja.

26 Ni baraka kwangu kuwa hapa na kuliona kanisa la Mungu likistawi, jengo jipya, na kadhalika. Mungu daima na awabariki ninyi watu! Iweni waaminifu kwa Kristo. Dumuni wakweli kwa mchungaji, na mfanye kazi pamoja, kila mtu bega kwa bega, kwa kuwa ninaamini Kuja kwa Bwana kumekaribia.

27 Sasa, kabla tu hatujalikaribia Neno, hebu tumkaribie Mwandishi katika maombi, tunapoviinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi tu.

28 Kabla tu hatujaomba, huku vichwa vyenu na mioyo imeinamishwa, kunayo haja humu kwa ajili ya maombi, nawe ungelitambulisha kwa mkono ulioinuliwa, moyoni mwako tu una haja ya kitu fulani, na kusema, "Bwana Yesu, unikumbuke"? Bwana anaona kila mkono. Nina hakika.

29 Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha sana ya kwamba tunaweza kukuita "Baba," Muumba mkuu wa mbingu na nchi, Elohimu mkuu, El-Shadai, Mpaji Nguvu, Mwenye kulisha,

Yeye atoshelezaye kwa yote. Na kupitia kwa Mwana Wako mwenyewe mpendwa, Yeye alitwambia: kama tungekuja Kwako, na kuomba lolote, tukilitumia Jina Lake, ya kwamba Yeye angehakikisha kwamba lilijaliwa. Na, Baba, tunaamini ya kwamba hilo liko kwa masharti. Kama tukiomba kitu kibaya, tusingeweza kuwa na imani kuamini ya kwamba kingejibiwa. Lakini kama tunaweza kuichunguza mioyo yetu usiku wa leo, hatuombi chochote kibaya, bali kilicho kizuri, hicho ni, kwamba Wewe utatusamehe dhambi zetu zote na makosa, kwa kuwa kweli, Bwana, hilo ndilo jambo la kwanza.

30 Hatutaki kujaribu kuingia katika Uwepo Wako tukiwa na dhambi juu yetu. Kwa hiyo, tukijua hilo, kila siku, shida na mambo yanayotuzonga, ambayo huenda hata yasionekane katika mawazo yetu wenyewe, bali, tunapokuja kuwazia juu ya Mungu mtakatifu, Yule ambaye hata Malaika ni wachafu mbele Zake, ndipo tunajua, Bwana, kwamba hata hatuna nafasi isipokuwa tupitie kwenye Damu ya Yesu Kristo, ndipo basi sisi ni watoto wa Mungu. Makosa yetu yanasamehewa, tunapoyakiri.

31 Nami naomba, usiku wa leo, Baba, ya kwamba Wewe utalibariki kusanyiko hili lililoinua mikono yao. Unajua kilichokuwa nyuma ya kila mmoja wa mikono hiyo: wazo, shauku, na—na nia na kusudi ya kuuinua. Ninaomba ya kwamba utajalia kila mmoja haja yao.

32 Na sasa, Baba, tunaliombea kanisa hili. Tuna furaha sana, ya kwamba, mahali hapa. Tunaposoma huko nyuma katika siku za mwanzoni, ambako Wakristo walichukiwa sana, hata wasingeweza kuwa na kanisa. Kwamba, walikuwa ni maskini sana, wasingeweza kujenga moja kama wangalikuwa nalo, na kuona hilo, ama, wangalikuwa na nafasi ya kufanya hivyo. Na sasa, leo hii, kuona mijengo mikubwa mizuri, ikijengwa, safi, walipo watu, wanaweza kuingia na kumwabudu Mungu. Tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili. Na kwa ajili ya kujitolea ambako, watu, pamoja na zaka zao na matoleo na—na michango, wameijenga nyumba hii kwa ajili ya Bwana.

33 Sasa, Baba Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utambariki mchungaji wake, mashemasi wake, wadhamini wake, na kila mshiriki ambaye huja hapa. Jalia likue, na kukua, na kukua. Pia jalia, kutoka kwenye kanisa hili, uibuke uamsho wa mtindo wa kale utakaoenea kwenye hili bonde, kabisa kabisa. Jalia kuwe na ishara na maajabu yatakayotoka kwenye kanisa hili, ya uponyaji, wokovu. Jalia liwe mnara wa taa kwa taifa lote. Lijalie, Bwana.

34 Jalia, kutoka mahali hapa, watoke wahubiri wazuri, vijana, wito wa Mungu maishani mwao, waende kwenye huduma za kimishenari, popote watakapoitwa. Lijalie, Bwana.

35 Na usiku wa leo, wakati tumekusanyika pamoja, jalia Roho Mtakatifu aje, aingie kwenye Neno, na kupanda tu Mbegu

katika kila moyo uliopo hapa ndani. Tujalie kwa imani tulitilie Hilo maji, mchana na usiku, mpaka litakapokua likawa miti mikubwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

36 Mponye kila mgonjwa, Bwana, aliye hapa usiku wa leo. Mwokoe kila mtu aliyepotea. Warejeshe wote waliorudi nyuma. Na uwafanye upya na kuwajaza tena wale ambao wamejazwa hapo kabla. Lijalie, Bwana, kwa kuwa tunaomba hili katika Jina la Yesu Kristo, Mtoto Wako. Amina.

37 Sasa, nimechelewa kidogo tu, kama kawaida. Muda ulikuwa umeenda zaidi kidogo huku usiku wa leo kuliko nilivyoutarajia kuwa.

38 Na kwa hiyo tuko, kesho usiku, mahali fulani. Nadhani tayari wamelitangaza. Na sasa, endapo mna kanisa kwenye kanisa lenu hapa, kesho usiku, msishuke kuja huku. Lakini ikiwa hamna kanisa, tungefurahia kuwa pamoja nanyi. Daima tunawataka watu wakae kwenye wajibu wao, kwa vyovyote vile. Kanisa linapofunguliwa, kila askari anapaswa kuwa katika cheo chake na mahali pake.

39 Na kwa hiyo tupo hapa tukitembelea na kuwa na wakati mzuri sana, kabla tu ya—ya mkutano mkubwa wa Wafanyabiashara. Na kama vile nimetangaza tayari, Ndugu Roberts anapaswa kuwa hapa kuifungua ibada, kwa ajili ya Alhamisi usiku. Tutafurahia sana kukutana na Ndugu Roberts. Halafu basi nafikiri, labda Ijumaa, Ndugu Velmer Gardner atakuwa hapa. Sijui kama atazungumza usiku huo, au la.

40 Nami nafikiri nimepangiwa huo, kuwa huko Jumamosi asubuhi, kwenye kiamshakinywa. Basi ikiwa ni mapenzi ya Mungu, na kwamba nizungumze Jumamosi asubuhi, ninataka kuchukua fungu, ikiwa, yakiwa ni mapenzi ya Mungu: *Mtu Mchoyo Kuliko Wote Niliyepata Kukutana Naye*. Kwa hiyo, na—na halafu, Jumapili alasiri, nitazungumza tena. Kwa hiyo kama nyinyi. . . Sasa, Jumamosi asubuhi, hakuna kanisa, nijuavyo mimi. Na Jumapili alasiri hakuna kanisa, nijuavyo mimi.

41 Sasa, kabla sijaanza, nilisahau nina . . . La. Ninaamini Billy alisema ya kwamba alisambaza kadi hizo zingine za maombi. Hiyo ni kweli? Kunazo kadi za maombi zilizosambazwa hapa usiku wa leo? Vema, alisambaza sehemu yake, kwenye kanisa lile lingine, jana usiku, kwa sababu ni—nimekuwa nikiwacheleweshaa watu sana.

42 Kidogo ninahubiri kwa muda mrefu, saa sita ama nane, kitu kama hicho, wakati mwingine, ninapomalizia. Sasa, sininii . . . Usiku wa leo, sikusudii kuhubiri zaidi ya nusu ya hizo. Ninii tu . . . Kwa hiyo nilifikiri tulisambaza kadi za maombi, na halafu sisi . . . mngeweza kwenda nyumbani kwenye usiku wa manane, kwa vyovyote vile, kwa hiyo basi tukiisha kufanyiza mstari wa maombi. Kwa hiyo, kama tu ni nusu ya hizo. Wala sijui sana, lakini hunichukua tu muda mrefu sana kusema yale

nijuayo. Kwa hiyo, yale nijuayo, ninapenda kuyasema vizuri sana, ninachukua tu muda wangu pamoja nayo, mwajua. Ni vema. Nilikuwa tu nikitania hapo, maana ni—nitajaribu kutoka, dakika zingine arobaini na tano, ama kitu fulani, kwenye mstari wa maombi.

43 Ninalo tu maskini, Andiko moja hapa usiku wa leo ninalotaka kusoma, na kuchukua somo, na kuomba ya kwamba Mungu atalibariki. Ukitaka kulisoma utakapofika nyumbani, ni katika Marko, mlango wa 10 na kifungu cha 28.

> *Petro* akaanza *kumwambia, Tazama, sisi tumeacha yote, tukakufuata wewe.*

44 Sasa, ningetaka kuchukua somo, kujenga muktadha mdogo juu pale, wa: *Kuacha Yote*. Halafu basi, katika dakika chache, tutawaombea wagonjwa. Na sasa, ninyi mnaoifahamu Marko, mlango wa 10, kuiwekea msingi. Ninii tu . . . Yesu alikuwa akizungumza, awali, juu ya talaka.

45 Halafu basi Yeye pia alikuwa na jambo la kustaajabisha sana lililotukia. Kulikuwako na kijana tajiri mwanamume aliyekuja Kwake mbio, na kusema, "Bwana Mwema, nifanyeje nipate Uzima wa Milele?"

Na Yeye akamwambia, "Zishike amri."

46 Huyo kijana mwanamume akasema, "Nimeyashika haya tangu utoto wangu." Ama, "Amri zipi?" Naye akamwambia zilikuwa ni zipi. Naye akasema, "Nimezishika hizi."

47 Akasema, "Ila umepungukiwa na neno moja. Ukitaka kuwa na Uzima wa Milele, kuwa mkamilifu, basi uza vyote ulivyo navyo ukawape maskini. Uuchukue msalaba wako unifuate."

48 Hebu tumfuatilie kijana huyo mwanamume kwa dakika chache kabla hatujaingia kwenye somo letu, kuweka msingi.

49 Sasa, mnaona, kijana huyo mwanamume aliombwa kuacha yote, bali akakataa kufanya hivyo. Na wakati mwingine kama tukitumia ufanisi na utajiri, na kadhalika, "mafanikio," lakini kijana huyu mwanamume alikuwa kijana mwanamume aliyefanikiwa na hata hivyo hakuwa na Uzima wa Milele. Kwa hiyo, wakati mwingine, mafanikio hayamaanishi kila mara kwamba Mungu anabariki.

50 Lakini hebu tumfuate. Tunamwona hapa sasa katika ujana wake, kijana, labda mwenye sura nzuri, mdogo, aliyevalia nadhifu. Biblia ilisema, ya kwamba, "Yesu alimpenda." Hana budi kuwa na dhamira njema, ya kupendeza, nyenyekevu. Hana budi kuwa kitu kizuri sa—sana, la sivyo asingeweza kuuvutia upendo wa Bwana Yesu. Kwa sababu, Yesu alipomtazama, "Yeye alimpenda." Hapana shaka alikuwa na sura nzuri, na mwonekano mzuri kwake, mwungwana safi, mvulana mwema. Basi akamwendea Yesu, labda akiwazia, katika uaminifu, na

kusema, “Ningetaka kujua yale ningeweza kufanya nipate Uzima wa Milele.”

51 Na wakati ilipombidi kutengana na yale aliyokuwa nayo, apate Uzima wa Milele, ndipo swali likawa langoni, kama unaweza kufaulu. Na swali hilo liko mbele ya kila mmoja wetu. Naye Yesu kweli alimwomba aachane na yote aliyokuwa nayo, auchukue msalaba wake, na kumfuata Yeye. Nasi tunaijua hiyo hadithi. “Aliondoka akiwa na huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.”

52 Ndipo Yesu akageuka, akasema, “Jinsi ingekuwa vigumu kwa mtu mwenye mali kuingia katika Ufalme wa Mungu, ni kama ngamia kupenya katika tundu la sindano. Lakini hiyo haingewezekana kwa mwanadamu, bali,” Yeye akasema, “kwa Mungu si lisilowezekana.”

53 Hebu tumfuatilie huyu kijana mtawala. Wakati mwingine tunapomwona, katika Biblia, yeye kamwe. . .mara alipoikataa nafasi ya kumfuata Yesu, wakati alipoelezewa kwa uzito sana.

54 Mnaona, tunataka kushikilia kila kitu tuwezacho, kisha tumfuate Yesu. Lakini wakati mwingine Yesu anatutaka tuachilie kila kitu, kusudi tuweke mikono yote miwili juu Yake. Wakati mwingine tunafikiri ya kwamba, kwa sababu tu kwamba—kwamba tumeshikilia.

55 Inanikumbusha juu ya kitu kidogo ninachosimulia kwa kawaida, juu ya wasichana wangu wawili wadogo. Hao sio wadogo sana sasa, ni wasichana wenye kimo kizuri sana. Lakini, walipokuwa wadogo. . .Mmoja wao ni Rebekah; yeye ndiye mwenye umri mkubwa zaidi. Naye, Sarah, ndiye mdogo. Naye Becky yuna macho ya samawati, na Sarah ana ya hudhurungi. Lakini wote wawili ni wasichana wa Baba, mwajua. Na kwa hiyo hungojea wanione nikija nyumbani, nao sikuzote wanapenda kuniona mimi. Basi kwa hiyo Becky kidogo ni . . . kidogo alikuwa msichana mrefu, mwembamba. Naye Sarah alikuwa mdogo, kidogo ni mfupi, jamaa mdogo.

56 Na kwa hiyo walikuwa wakiningojea mimi nije nyumbani, usiku mmoja. Nilikuwa nje mikutanoni, nao walijua ningekuja nyumbani, kwa hiyo wakawazia wangengojea tu kidogo. Na kama nikija nyumbani, walitaka kuniona. Vema, mwanamchanga hapana shaka aliwanyunyizia mchanga machoni mwao, nao wakashikwa na usingizi. Na hatimaye wakaenda kitandani, huko chumbani mwao.

57 Nami nikafika nimechelewa. Kwa hiyo nikaingia, nilikuwa nimechoka sana, nikaenda kulala. Na baada ya mikutano, na kadhalika, mimi huchoka sana siwezi kulala, baada ya majuma machache ya mikutano. Basi nikalala yapata saa mbili ama tatu, nikaamka, nikaenda se—sebuleni, nami nikaketi tu kitini. Nilikuwa nimeketi pale kitini, asubuhi na mapema.

58 Ndipo baada ya kitambo kidogo, Becky akageuka, katika chumba chake cha kulala, naye akatambua kulikuwa kumepambazuka. Ndipo akachungulia sebuleni, naye akaniona nimeketi hapo kitini. Huyo akatoka kitandani, upesi tu alivyoweza, maskini miguu hiyo mirefu, iliyokonda, ikitimua mbio tu.

59 Vema, hilo—hilo lilimshtusha Sarah. Nami sijui kama watoto wenu hufanya hivyo, au la, lakini, wangu, ukimnunulia kitu yule mkubwa, basi wa pili hupata cha kupokezanwa. Basi Sarah alikuwa amevalia pajama ya Rebekah, miguu mikubwa sana, mwajua, nayo ni kubwa mno kwake. Basi, yeye, huyo akatoka kitandani, huku hiyo miguu mikubwa ikipeperuka. Naye ilikuwa ni vigumu kushindana na Rebekah.

60 Kwa hiyo Rebekah akamtangulia kunifikia. Kisha akaruka pajani mwangu, akanikumbatia kwa mikono yote miwili, kidogo kuninii tu. . . Alikuwa kwenye goti langu la kulia, nayo miguu yake mirefu imefika sakafuni. Alikuwa na uwiano mzuri sana.

61 Kidogo inanikumbusha juu ya baadhi ya yale madhehebu ya kwanza makubwa zaidi, mwajua, yaliyoibuka. Mwajua, yamekuwa hapa muda mrefu, kidogo yana miguu mirefu, na kadhalika, yana uwiano mzuri sana.

62 Basi huyu hapa Sarah anakuja, lile kanisa dogo, changa, mwajua, ambalo halijakaa muda mrefu sana. Naye kwa namna fulani aliona ya kwamba Becky alikuwa amemtangulia—amemtangulia pale.

63 Kwa hiyo Rebekah alikuwa amenikumbatia. Akaangalia kote. Akasema, "Sarah, dada yangu, ninataka ujue jambo moja." Akasema, "Nilikuwa wa kwanza hapa." Kisha akasema, "Ninaye baba wote, wala hakuna kilichosalia kwa ajili yako." (Wao wanajaribu kutwambia hivyo, mwajua, wakati wote.) Kasema, "Nilitangulia hapa, nami ninaye baba wote, wala hakuna kilichosalia kwa ajili yako."

64 Maskini Sarah mdogo akakiinamisha kichwa chake chini. Mdomo wake mdogo ukashuka. Akaanza kuondoka, na machozi katika macho hayo makubwa ya hudhurungi. Naye Becky alikuwa amekilaza kichwa chake begani mwangu, kidogo akinikumbatia.

65 Nikakichukua kidole changu na kuashiria namna *hiyo,* kwa Sarah, kisha nikautokeza mguu huo mwingine. Huyu hapa anakuja, naye akaruka juu ya mguu huo mwingine, na, mbona, a—a—asingeweza kujisawazisha. Miguu yake midogo isingeweza kufika sakafuni. Bali alikuwa mguuni, kwa vyovyote vile. Mnaona? Kwa hiyo alikuwa akidemadema namna *hiyo*.

66 Vema, kumzuia asianguke, nilichukua tu mikono yote miwili na kumkumbatia kwayo, namna *hiyo,* kumshikilia. Nami nilikuwa nimemvuta kwangu, naye akakiweka maskini kichwa chake kwangu muda kidogo.

67 Akainuka na kumwangalia Becky, kisha kasema, "Sasa, Rebekah, dada yangu," kasema, "Ninataka kukwambia jambo fulani, pia." Akasema, "Huenda ikawa kweli kwamba unaye baba wote, bali nataka ujue ya kwamba baba yuna mimi wote." Kwa hiyo hiyo ni kweli.

68 Kwa hiyo hivyo ni kama jinsi tunavyotaka. Hatutaki... Tunamtaka Yeye awe nasi wote. Kwa hiyo, basi, katika yote, kufanya hivyo, hatuna budi tu kutembea kule kwa imani na kumwamini Yeye, hivyo tu, na kutumaini tu. Hatuwezi kulielezea. Hakuna njia ya kulielezea. Tunaliamini tu, na kulichukua namna hiyo.

69 Kijana mwanamume huyu tajiri, asingejitolea kwa Kristo, na kwa hiyo aliondoka. Ndipo tunamwona, baadaye, kwamba alikuwa...Alikuwa amefanikiwa sana, mpaka maghala yake yalikuwa yamejaa, hata yeye akasema, "Ewe nafsi, starehe." Loo, alikuwa amesitawi, kila kitu. Alikuwa na nyingi sana, hakuwa na haja ya kitu.

70 Lakini jambo fulani lilitukia. Wakati mwingine tulipomwona, aliyainua macho yake katika kuzimu, ambako alimwona yule ombaomba huko mbali sana kifuani mwa Ibrahimu. Hiyo ilikuwa ni kwa sababu hakuwa tayari kuacha yote, kumfuata Bwana Yesu.

71 Halafu, jambo hili lilipotukia, naye huyo mtawala kijana asingesalimisha yale aliyokuwa nayo, apate kumfuata Yesu, hapana shaka Petro alianza kuelewa. Ninaamini yeye ndiye aliyetoa tamshi hilo, ama aliyeuliza hilo swali, aliyelileta. Ndipo akasema, "Sasa, tumeacha yote, kukufuata Wewe. Tumeacha yote. Angalia yale tuliyofanya. Tuliyaacha makazi yetu. Tuliziacha familia zetu. Tuliyaacha mashamba yetu. Tuliacha kila kitu tulichokuwa nacho, kukufuata Wewe."

72 Ikaanza kumfunukia. Labda alikuwa ameshikwa sana na kazi, akimwangalia Kristo, na kadhalika, hata yeye...Kamwe halikuwa limemfunukia, kwamba alikuwa ameyaacha makazi yake. Alikuwa ameiacha familia yake. Alikuwa amemwacha baba yake, mama yake. Alikuwa ameyaacha yote aliyokuwa nayo, apate kumfuata Yesu.

73 Bali hilo hasa ndilo Mungu analohitaji: kuacha yote na kumfuata Yeye. Hayo ndiyo matakwa ya Mungu. Hatuna budi kufanya hivyo pia. Wakati mwingine inatubidi kuacha mawazo yetu yenyewe. Ikiwa mawazo yetu juu ya chochote ni kinyume na Neno la Mungu, inatubidi kuacha mawazo yetu wenyewe na kumfuata Yeye. Na njia pekee tunayoweza kumfuata Yeye ni kulifuata Neno Lake, kulitii. Nalo ombi la Mungu na matakwa ya Mungu ni kwamba tuache yote na tumfuate Yeye.

74 Lakini katika kufanya hilo, tunaona, wakati mwingine, inatubidi kuachana na marafiki zetu. Mara nyingi hilo ni jambo gumu kufanya. Sasa, watu wengi, wanapomjia Kristo

kwa mara ya kwanza na kujazwa na Roho, labda, kama vile wanawake, wamekuwa na namna fulani ya karamu wamekuwa wakihudhuria, kila usiku *fulani*, ambako wamekuwa wakicheza karata katika ujirani. Wamefahamiana na majirani wo—wote, na kadhalika, nao ni wa mashirika fulani katika ujirani, nao wanaenda, wanacheza karata. Nao wanawake hawa, mwajua, watasema jambo fulani kulihusu. Hawatalifahamu. Lakini, hata hivyo, huna budi kuachana na kitu hicho, kwa kuwa si vizuri kubahatisha, kucheza kamari. Nawe huna budi kuachana nazo kama ukimfuata Kristo.

75 Wakati mwingine wanawake, katika makanisa yetu, ambao wamezoea kuvaa nguo za kizinifu, kama vile kaptura, na—na hizi dangirizi. Nayo Biblia ilisema, "Ni chukizo kwa Mungu, kwa mwanamke kuvaa kama hizo." Yeye, haidhuru anawazia nini, hana budi kuachana na hizo. Wakati mwingine tunawaona wanawake, wanapokuja kwenye Njia na wanaokoka, wamezoea kukata nywele zao. Nao wanataka kuwa maarufu kama walimwengu wengine. Bali wanakuta, ni jambo gumu, maana watakuita wa mtindo wa kale, wakati wowote unapoanza kuvaa kama Mkristo, kutenda kama Mkristo, kuishi kama Mkristo. Watakuita wa mtindo wa kale, bali inakubidi kuacha yote, upate kumfuata Yeye.

76 Yesu alisema, ama Maandiko yanasema, "Yeye aupendaye ulimwengu, au mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yake." Kweli. Inahitaji, kuacha yote.

77 Hapo, unapokuwa tayari kuacha yote na kumfuata Yeye, basi, "Mkikaa ndani Yangu, nalo Neno Langu ndani yenu, mwaweza kuomba mtakalo nanyi mtafanyiwa." Lakini, huwezi, ukijua ya kwamba mambo hayo ni mabaya. Unajua ni mabaya.

78 Biblia inayapinga: kucheza karata, kuvuta sigara, kunywa pombe, kuvaa nguo za kizinifu. Na, halafu, kudai kuwa ni Mkristo. Iwapo hiyo roho iliyo ndani yako haiyahukumu hayo, basi kuna kasoro na roho iliyo ndani yako. Kwa sababu, Mungu Yule aliyeliandika Neno ndiye hilo Neno. Nalo hilo Neno liko ndani yako, Nalo linakuhukumu. Halina budi kukuhukumu. Basi iwapo halikuhukumu, unadanganyika. Roho Mtakatifu anawezaje kuandika kitu fulani, nawe ugeuke na kufanya kinyume Chake, na kusema Roho Mtakatifu anakuongoza? Huwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, kuvuta sigara, kunywa wiski, kucheza karata, kukata nywele, kuvaa kaptura, mambo haya mengine yote, ni makosa, ni dhambi mbaya, na kamwe hutafika popote mpaka utakapoachana nayo.

79 Yananyemelea kwenye huduma zetu za Kipentekoste. Aibu kwenu. Mnapaswa kujionea aibu. Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho wa ulimwengu mzima. Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho wa kipentekoste. Jambo fulani limetukia. Hiyo ni kweli.

Tumelegeza vizuizi, ndipo mambo yanatukia ambayo hayapaswi kutukia. Kwa hiyo hamna budi kuacha yote, kumfuata Kristo.

80 Huna budi kuacha yako, mawazo yako mwenyewe. Inakubidi kuambatana na Neno Lake. Wala kamwe Roho Mtakatifu hatakana Neno lolote alilowahi kunena. Nayo Biblia imeandikwa na Roho Mtakatifu. Biblia ilisema hivyo. Na ikiwa . . . Maneno ya Biblia ni Mungu. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu."

81 Sasa Neno limefanyika Roho, anaishi ndani yetu, "Kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi ukamilifu wa dahari, ule ukamilisho." Sasa, kama Mungu yule yule aliyeiandika Biblia yuko ndani yako, wewe si mali yako, umekufa kwa mambo ya ulimwengu, umekufa kwa mawazo yako mwenyewe, na "nia ambayo—nia ambayo ilikuwamo ndani ya Kristo iwe ndani yako." Hapo, basi unayaacha yote, upate kumfuata Yeye. Sio mawazo yako mwenyewe; yale Yeye asemayo. "Si mapenzi Yangu; Yako, Bwana." Ndipo unaanza kujilainisha na Neno la Mungu.

Tungeweza kukaa hapo muda mrefu, bali nitaendelea mbele kidogo.

82 "Lakini," unasema, "ninapata nini basi, nikiacha yote? Kuacha yote, ninapata nini?"

83 Unaweza kuutarajia ulimwengu kukudhihaki. Unaweza kuutarajia ulimwengu ukuite kila namna ya majina ya aibu. Watakuita chochote wanachoweza kukuita. Utadharauliwa na kukataliwa.

84 Yesu, kwa sababu ya Yeye kuwa Imanueli, Mungu akiishi ndani Yake, ilimfanya Yeye wa kipekee sana kwa kanisa Lake mwenyewe hata kanisa Lake mwenyewe likamfukuza mara Yeye alipoingia. Hao ndio waliomtundika msalabani. Hao ndio waliomhukumu. Yeye aliwapenda watu. Moyo Wake wote ulikuwa kwa watu. Lakini ilimbidi kuacha kila kitu, kusudi amfuate Mungu.

85 Na vivyo hivyo inatupasa kuacha kila kitu, ili tumfuate Mungu.

"Sasa, ninapata nini kama malipo?" Hatutarajii . . .

86 Sisi, wakati mwingine, nafikiri sisi wahudumu tunalifanya kidogo kuwa maua kupita kiasi kwa mwo—mwongofu. "Loo, njoni kwa Kristo, kila kitu ni cha kupendeza." Lakini, mnaona, sivyo ilivyo, kwa njia hiyo, huko kusema kwamba kila kitu ni raha mstarehe. Kwa sababu, hakuna Mkristo . . .

87 Biblia ilisema, "Wote wanaoishi maisha ya kitauwa katika Kristo Yesu watateswa." Kwa hiyo kama—kama huteswi kwa ajili ya Kristo, basi kuna kasoro.

88 Iwapo ibilisi hakufuatilii, amekupata. Hakuna lingine, kwa sababu mradi tu yeye anakufuatilia, hiyo ni ishara hajakupata bado. Lakini kama hakufuatilii, ni ishara yeye amekupata. Naam. Kwa hiyo kumbuka tu, mradi tu anakushambulia, uko hatua chache mbele yake bado, basi endelea tu kusonga mbele.

89 "Lakini wote wanaoishi maisha ya kitauwa katika Kristo Yesu watateswa." Yeye alisema, "Furahini na kushangilia, kwa kuwa ndivyo walivyowatesa manabii waliokuwa kabla yenu." Hiyo ni kweli.

90 Usiende na uso uliokunjwa, na kusema, "Vema, sikupaswa kufanya hivyo. Nadhani, wao—wao, kamwe siwezi kuvumilia mtu kunena habari zangu, na kusema mimi ni wa mtindo wa kale, mimi ni *hiki, kile,* ama *kinginecho*."

91 Loo, u—unapaswa kuwa mwenye furaha sana, ulifurahie, kwa sababu unaweza kuchukua shutuma la Jina Lake. Na kwa kushika amri Zake, ilikufanya ufanye hivyo.

92 Ila ninataka kusema jambo hili, pia. (Nitaharakisha, upesi tuwezavyo.) Mungu kamwe, kwa vyovyote vile, hatakuwa na deni ya mtu yeyote. Mungu hatakuwa na deni ya mtu yeyote. Kama umemfanyia Mungu hilo, ukaacha yote, Mungu atakulipa mara elfu. Kweli. Mungu atalipa. Ukiacha mambo ya ulimwengu, na ulimwengu, na mambo ya ulimwengu, basi Mungu atakulipa mara nyingi sana.

93 Ni wangapi walio mashahidi wa hilo, hapa usiku wa leo? Vema, sote tunajua ya kwamba Mungu atalipa.

Sasa hebu tuwachukue tu watu wachache ambao kweli waliacha yote.

94 Hebu tumchukue, kwanza, baba wa imani, Ibrahimu. Ibrahimu aliiacha nchi yake mwenyewe, mali aliyokuwa nayo, na kila kitu kingine. Yeye aliitwa kutoka Ukaldayo, mji wa Uri. Basi akaiacha nchi yake, makazi yake, watu wake, na wote, na kumfuata Mungu. Ilimbidi kuacha kila kitu, kukiacha nyuma. Akaiacha nchi ya—yake, mali yake huko Ukaldayo, katika Uri. Akaiacha mali yake, ndipo Mungu akampa nchi yote iliyoahidiwa. Mungu hulipa pamoja na riba kubwa. Yeye alimpa, huko juu siku hiyo, hapo alipokutana naye, Yeye alisema, "Simama, Ibrahimu. Angalia mashariki, kaskazini, magharibi, kusini, ninakupa yote, yote ni yako."

95 Hiyo ndiyo shida ya Wakristo usiku wa leo. Mungu hutupa sisi, bali tunaogopa kuichunguza. Unapokuwa Mkristo, wewe ni mrithi wa kila ahadi iliyo katika Biblia. Hiyo ni kweli. Kila kitu ambacho Mungu aliahidi, ni chako. Ni kama tu njia tao kubwa mno, na kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika njia tao hii, ambayo ni Kristo. Vema, endapo mimi . . . Kama mtu akinipa kitu, nitaangalia kote kuona yaliyo yangu.

96 Nafikiri hivyo ndivyo Wakristo wanavyopaswa kufanya usiku wa leo. Tafuta kujua uliyo nayo. Kama kitu kikienda juu zaidi tu kidogo, hata nisiweze kukifikia, nitajitafutia ngazi ya vipandio nipande nikifikie. Na kama kitu fulani kinaonekana hakifikiliki, katika Biblia, ambacho Mungu amekiahidi, nitakaa magotini mwangu na kuipanda ngazi ya Yakobo mpaka nikifikie, maana ni changu. Mungu alinipa hicho.

97 Ikiwa uponyaji wa Kiungu umeahidiwa katika Biblia, nami ni mgonjwa, nitakaa hapo mpaka Mungu anipe mimi, maana ni ahadi. Mungu aliahidi ningeuacha ulimwengu, Yeye akanipa Roho Mtakatifu, nitakaa hapo hapo mpaka atakaponipa Huyo, kwa sababu Yeye aliahidi. Kama Mungu aliahidi kunipa shauku ya moyo wangu, nayo shauku ya moyo wangu ni kitu kizuri, nitakaa hapo mpaka Mungu anipe, kwa sababu ni ahadi. Nami nimeuacha ulimwengu wote. Ninataka kumfuata Yeye, na Yeye atalipa. Ninajua hiyo ni kweli. Ni kweli kabisa.

98 Yeye alifanya nini? Aliacha shamba lake, taifa lake. Naye Mungu akampa jimbo zima, ama yote, bara lote la. . .la Palestina. Yeye alikiacha kijipande chake kidogo cha shamba huko chini, labda ekari moja ambapo nyumba yake ilikalia, na nyumba yake ya siku nyingi, apate kupokea kila kitu kilichokuwa katika Palestina. Vema.

99 Lakini kitu cha kwanza alichopaswa kufanya ni kujitenga mwenyewe. Alijitenga na watu wake, wapendwa wake wote, wenzake wa zamani aliozoea ku—kutembea nao kote, marafiki zake wa ujanani walioshuka kutoka Babeli, pamoja naye, na ndugu zake wote, dada, na marafiki zake wote aliowafahamu, wenzake. Mungu alipomwita, Yeye alisema, "Jitenge na ukoo wako. Yaondokee yote hayo." Sasa, hilo lilikuwa gumu, bali yeye alijitenga na jamaa zake wote. Kwa nini? Kwa sababu wasingekubaliana naye.

100 Ungeweza kuwazia wakikubaliana? Mwanamume mkongwe hapa, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, na mke mwenye umri wa miaka sitini na mitano, akisema, "Unajua nini? Nilikutana na Mungu hapa nje na Yeye akaniambia nitampata m—m—mtoto sasa, kwa Sara."

101 Mbona, wao, daktari rafiki yake, angalisema, "Huyu mzee amerukwa na akili." Lakini tayari alikuwa amenunua pini na jichondege, na kila kitu kingine, akijiandaa kwa ajili yake, kwa sababu alijua atampata. Hiyo ni kweli. Hakuna kitu kwake. Kwa nini? Mungu aliahidi jambo hilo. Kweli.

102 Basi endapo kundi hilo la watu lilitaka kumcheka na kufikiria alikuwa amerukwa na akili, wanamfanyia kila mwaminio hivyo. Uzao wote wa Ibrahimu unalo jambo lilo hilo. Hiyo ni kweli. Wakati mwingine kanisa lako hata litakufukuza. Vilabu vyako, mahali pa—pako unaposhiriki, ushirika wako katika ujirani, wenzako. Wakati mwingine rafiki yako wa kiume

ama rafiki yako wa kike atakukataa. Lakini Mungu anakutaka uache yote, upate kumfuata Yeye. Acha kila kitu kilicho kinyume na Yeye, ukamfuate.

103 Sasa, Ibrahimu, akiwaacha watu wake, yeye alipata nini nyuma yake? Ni kitu gani kilichokuja kando na hilo? Akawa baba wa mataifa mengi. Mungu alimfanya baba wa mataifa mengi. Yale machache aliyoyaacha, kisha angalia kile alichofanyika. Yesu alisema, "Yeye atakayeacha . . . Mimi, atakuwa na baba, mama, na kadhalika." Angalieni kile Ibrahimu alichopata, kwa kuacha yote na kumfuata Yeye. Naam, bwana. "Baba wa mataifa mengi."

104 Lakini, kwanza, ilimbidi kujitenga mwenyewe na kutokuamini kwote, na hata na ndugu yake mfuasi baridi, vuguvugu, wa kanisa, Lutu. Ilimbidi kujiacha mwenyewe, kwa ajili yake.

105 Kila kitu kilicho na kutokuamini ndani yake, inakubidi kujitenga; chochote kile, kama ni kanuni ya imani, kama uko katika kanisa, na yote unayotegemea ni kanuni ya imani, wala huliamini Neno, na kama Neno ni kinyume na . . . Kanuni ya imani ni kinyume na Neno, itakubidi kuacha hiyo. Itakubidi kuacha kila kitu.

106 Na Mungu kamwe hakumbariki Ibrahimu mpaka alipomtii kikamilifu. Ibrahimu alitaka aende pamoja na baba yake, naye huyo mzee alikuwa ni tatizo, wakati wote. Hatimaye, akafa. Ndipo, Lutu, kulikuwako na ugomvi na kila kitu. Ndipo basi wakati Ibrahimu alipomtii Mungu kikamilifu na kujitenga mwenyewe, na kumwacha Lutu ashuke aende kule kwenye nchi nzuri, popote alipotaka kwenda, huko chini Sodoma, ndipo Mungu akamtokea Ibrahimu, na kusema, "Inua macho yako. Ninakupa wewe kitu hicho chote."

107 Ibrahimu ndiye aliyejitenga. Yeye ndiye aliyejitenga na yote, kufuata, kumfuata Mungu. Naye ndiye baba wa Imani. Yeye ndiye tunayeamini kuwa ni mwaminifu. "Ahadi ilifanywa kwa Ibrahimu na Uzao wake. Sisi tukiwa tumekufa katika Kristo ni uzao wa Ibrahimu, warithi pamoja na Yeye sawasawa na ahadi."

108 Israeli iliiacha Misri. Waliziacha nchi za kale huko chini Misri. Wapate kupokea nini? Palestina. Walitoka mahali pale pabaya sana huko chini Misri, wanyapara.

109 Na kuna watu wengi leo hii, wasichana huko nje mtaani, wakivuta sigara, wakinywa pombe, kama tulivyoona hapa kwenye—kwenye redio, hivi majuzi. Ilibidi hawa polisi waje na kulikamata kundi hilo la wasichana huko chini, huko mtaani, walioingia wazimu pamoja na maskini roho hiyo ya kale ya ibilisi, iliyowaingia kufanya hii bugibugi mpya, chochote wanachokiita kitu hicho, na huko nje mtaani, wameingia kichaa akilini mwao. Mnaona? Kweli, kama msichana ana wakia wa

uadilifu nafsini mwake, yeye ama kijana mwanamume, yeyote yule, kitu hicho ni mnyapara anayewasukuma kufanya hivyo.

110 Yaache hayo, na Mungu atakupa dansi. Loo, jamani! Hakika atakupa. Atakupa moja, ikiwa tu utaacha hayo. Ila inakupasa kuacha mambo hayo yote, kuipata. Kamwe huwezi kuendelea na zote mbili.

111 Alipata Palestina, Ibrahimu alipata, ama Israeli ilipata. Yeye aliipata nchi ya Palestina. Waliiacha ile nchi ya kale huko chini, nao wakaipata Palestina, nchi iliyojaa maziwa na asali. Naam, bwana.

112 Waliacha nini? Waliliacha hilo jua kali, chini ya mnyapara huko chini Misri. Walipata nini, kwa kuliacha hilo jua lenye joto huko chini? Walipata kutembea katika Nuru ya ile Nguzo ya Moto. Wakiliacha jua hilo kali huko chini, wapate kutembea katika Nuru ya Nguzo ya Moto ya Mungu. Ni badilisho la jinsi gani! Ningetaka kuchukua badilisho hilo, nanyi je? Nguzo ya Moto. Kutembea katika nuru ya jua la kawaida, ambako walikuwa wakitaabika chini ya wanyapara, kutoka huko nje na kutembea katika Nuru ya Mungu, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, Nguzo ya Moto iliyokuwa ikiwangoza kwenye nchi ya ahadi.

113 Jambo lile lile siku hizi. Kutembea kutoka katika mwangaza wa ulimwengu huu, mambo yaliyo ya ulimwengu, kutembea katika Nuru ya Mungu. Inakuongoza kwenye nchi ya ahadi.

114 Pia waliviacha maskini vyungu vya vitunguu saumu vya Misri, vyungu vya nyama huko Misri. Walipata nini walipoviacha maskini vyungu hivyo vya nyama? Walipata kula chakula cha Malaika. Mana ilishuka kutoka mbinguni, kupachukua mahali pa kitunguu saumu.

115 Sasa, kama hujawahi kula chochote ila kitunguu saumu, hebu nikwambie jambo fulani, Mungu yuna Mbingu iliyojaa Chakula cha Malaika, kukulisha. Hiyo ni kweli.

116 Chakula cha Malaika, hicho ndicho walichopata badala ya hivyo, badala ya maskini vitunguu saumu vya Misri.

117 Waliyaacha maji ya Misri yaliyojaa matope. Walipata nini huko nje? Kunywea ule Mwamba uliopigwa huko nyikani, wa maji safi sana ya Mungu. Waliyaacha maji ya Misri yaliyojaa matope, yale maji ya juu chini yaliyojaa matope ya kimadhehebu.

118 Hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya wakati mwingine siku hizi. Kuachana na kanuni hiyo ya kale na dhehebu, linalosema, "Siku za miujiza zimepita. Jamaa hao wana kichaa. Hao ni kundi tu la watakatifu wanaojibingirisha." Yaacheni hayo nyuma, mje huku mkanywe kutoka kwenye Chemchemi iliyojaa... iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambamo wenye dhambi

wakitumbukizwa chini ya hilo gharika hupoteza waa lao lote la hatia. Naam, bwana.

119 Yaacheni hayo maji ya kale ya matope, yaliyochanganyikana kabisa na mashaka, na vurugu, na ubishi, na ugomvi, na kila kitu kingine, na kushuka usiku na kufanya mlo wa supu, na kuchemsha maskini kuku na kumuuza senti hamsini, kwa sahani, mpate kumlipa mhubiri. Wakati, kama mngekuja huku chini ya sheria za Mungu, na amri takatifu za Mungu, na kutembea na Mungu, mtalipa zaka zenu, naye mhubiri ataendelea vizuri, kama mtaichukua tu njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo. Kweli. Maji ya kale yaliyojaa matope; mpate kuunywea ule Mwamba.

120 Wao waliwaacha huko chini hao matabibu wenye kujigamba wa Misri, wakisema, "Sisi ndio watu werevu kuliko wote ulimwenguni siku hizi." Waliwaacha hao matabibu wenye kujigamba, wapate kuwa na yule Tabibu Mkuu. Amina. Ningetaka kumwona tabibu fulani siku hizi akiendelea kama Tabibu yule Mkuu alivyofanya. Hao watu walikuwa nyikani kwa muda wa miaka arobaini, nao wakatokea pasipo na mtu mmoja mnyonge miongoni mwao. Hapakuwapo na mtu mnyonge miongoni mwao, miaka arobaini. Kulikuwako na zaidi ya watu milioni mbili waliotoka wakati huo. Ni watoto wachanga wangapi wanaozaliwa kila usiku? Ni wagonjwa wangapi? Nao walininii . . .

121 Ningetaka kwenda kwa Dk. Musa, na kuangalia kwenye mkoba wake, nione ni maagizo ya aina gani aliyowapa. Hivi si mngetaka kuona hilo? Nafikiri kuna madaktari wengi wangetaka kuangalia kwenye maagizo hayo. Vema, ninaweza kuwaambieni. Nimeyasoma. Mnataka niwaambie ni yapi? "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote." Hayo ndiyo yote aliyokuwa nayo. Hayo ndiyo yote aliyohitaji, kwa kuwa waliyaacha matatibu wenye kujigamba, wapate kuwa pamoja na Tabibu Mkuu. Naam, bwana.

122 Waliwaacha huko chini, hao watu waliosema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama miujiza, tena." Waliwaacha hao, wapate kufanya nini? Walifanya nini basi? Wapate kuwa papo hapo ambapo miujiza ingetukia, siku baada ya siku. Amina.

123 Watu siku hizi wanaosema ya kwamba hakuna kitu kama mwujiza, akili zao zina kasoro fulani. Hiyo ni kweli.

124 Mtu mmoja aliniambia, wakati mmoja, kasema, "Nisingejali unayofanya. Sikujali. Siwezi, haidhuru una thibitisho kiasi gani," kasema, "Siliamini kabisa."

125 Nikasema, "Bila shaka usingeamini. Usingeweza kuliona kamwe. Wewe ni kipofu kupita kiasi kuliona." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Hilo si kwa ajili ya wasioamini. Ni kwa ajili ya waaminio. Waaminio huliona." Hiyo ni kweli.

126 Jamaa mmoja aliniambia, wakati mmoja, alikutana nami mtaani, kasema, "Umekosea katika Fundisho lako."

Nikasema, "Ni Biblia."

127 Akasema, "Umekosea." Akasema, "Basi, sikubaliani nawe." Kasema, "Basi nipige kwa upofu. Paulo alimpiga mtu kwa upofu wakati mmoja." Kasema, "Nipige kwa upofu."

128 Nikasema, "Si—si—siwezi kufanya hivyo. Wewe tayari ni kipofu. Naam. Wewe ni . . . Ninawezaje kufanya yale baba yako, ibilisi, amefanya tayari?" Hiyo ni kweli. "Wewe tayari ni kipofu." Mtu anayesema jambo kama hilo, ni—ni kipofu sana, haijui nuru ya mchana kutoka kwa giza. Hawezi kutenganisha hizo mbili, Uzima au mauti. Huko ni kuwa kipofu kwelikweli. Naam, bwana. Naam.

129 Yule Tabibu Mkuu alikuwa pamoja nao, nao wakaiona miujiza ikifanyika. Hakika.

130 Wale wanafunzi, waliacha nini? Walikuwa na nyavu, nyavu za samaki. Waliziacha nyavu zao za samaki, wapate kutembea pamoja na Yeye, na kuona ishara Zake, na miujiza, na nguvu Zake, za kuwa Masihi. Mtu yeyote ambaye hangeacha uvuvi wa siku moja, apate kulifuata hilo, kuna kasoro fulani. Waliziacha nyavu zao, zilizojaa samaki. Wakaanza kuvuta, nao walikuwa na mvuo mkubwa kuliko wote waliowahi kuwa nao. Nao wakaacha kila sehemu yake, wapate kumfuata Yeye, kwa sababu waliamini moyoni mwao ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Nao walitaka kumfuata Yeye, wapate kuona kama hizo ishara zingemfuata Yeye kama Masihi. Nao wakaziona.

131 Ningeacha chochote kile ulimwenguni, sijali ni kitu gani, nipate kumwona Yesu Kristo akijidhihirisha Mwenyewe, hasa sana wakati imedhihirishwa maishani mwangu, kwamba ninajua nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani, nami ninajua kwamba Yeye ndiye Masihi. Ninajua, kwa kumwamini Yeye kwa Neno Lake, ya kwamba Yeye ameniokoa na maisha ya dhambi. Nami ninajua ya kwamba Roho Mtakatifu huishi ndani yangu. Ninaziona ishara Zake, kila mahali, zikielekeza, kwamba ninajua kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kuacha yote, niko tayari kuacha yote.

132 Mimi nilikuwa mfuasi wa dhehebu zuri, kanisa zuri, moja ya yaliyo mazuri kuliko yote nchini. Lakini wao walisema, "Billy, utarukwa na akili na kuwa mtakatifu anayejibingirisha."

133 Papo hapo, nikasema, "Afadhali mwichukue kadi yangu ya ushirika sasa hivi, kwa sababu nitamfuata Roho Mtakatifu." Hiyo ni kweli. Kweli.

134 Nawe huna budi kuacha kila kitu, hiyo ni kweli, kumfuata Yeye. Lakini yeye atakayeacha yote, na kumfuata Yeye, Mungu hulipa katika wingi wa baraka za utajiri. Hakuna kitu cha kulinganisha nazo. Vema.

135 Sasa, wale wanafunzi waliziacha nyavu zao, na nyavu za samaki zilizojaa samaki, biashara yao. Waliacha biashara yao, wapate kumfuata Bwana Yesu, kuziona nguvu Zake, kuiona ile ishara. Hao watu walikuwa ni watu waliofunzwa. Wanajua kile Masihi alichopaswa kufanya. Walikuwa wamesoma, huko nyuma kwenye Biblia. Walifahamu kile hasa Masihi atakachofanya. Walijua wakati wake wa kutukia ulikuwa umewadia. Ndipo walipomwona Mtu huyu amejitokeza jukwaani, Yule aliyetimiza hilo, basi walikuwa tayari kuacha kila kitu, wapate kusikia yale Yeye aliyotaka kusema. Maana, kama ilikuwa ni Masihi, basi ilikuwa ni Uzima kwao, kwa sababu walikuwa wamealikwa kumfuata Yeye. Kwa hiyo waliacha kila kitu.

136 Ndivyo ilivyo leo hii, kama *Huu* ni kweli, kama Ujumbe huu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho, ambapo alisema Yeye angeimwaga mvua ya masika na mvua ya vuli juu yetu. Iwapo mambo haya ni ya kweli, inafaa kuacha kila kitu. Tuufuate Huo.

137 Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Kweli.

138 "Enendeni ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, watashika nyoka. Wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hivyo ndivyo Yeye alivyosema.

139 "Kama Baba alivyonituma Mimi, ndivyo Mimi ninavyowatuma." Baba aliyemtuma huyo Mwana, aliambatana na huyo Mwana, na alikuwa ndani ya Mwana. Yesu anayemtuma mtu, huambatana naye, na yuko ndani yake, kutenda na kufanya kazi zile zile. "Lo, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari. Nazo kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya."

140 Ndugu, kama hilo si zuri kuliko kanuni za kale za imani na upuuzi wa ulimwengu, na kuwa mfuasi wa lingine kule linaloyakana yote Hayo! Mbona, nafikiri tunapaswa kuwa watu wenye furaha sana kuliko wote ulimwenguni, kumwona Mungu aliye hai akitembea karibu nasi namna hii; tukijua ya kwamba tumeacha yote, tupate kumfuata Yeye. Amina. Hilo linanifanya nijisikie kubarikiwa. Kuacha yote, kumfuata Bwana Yesu. Vivyo hivyo leo hii, huna budi kuacha yote. Kama tu walivyofanya huko nyuma, inakupasa kufanya, pia.

141 Sasa, mnazungumza kuhusu mtu fulani kuacha kitu fulani, hebu tuangalie yale, kwa ajili ya Yesu, Yesu aliyoacha kwa ajili yetu. Yesu alisalimisha kila kitu. Alikuwa na makao Mbinguni. Na Yeye akayaacha makao Yake Mbinguni, akaja duniani, wala hata hakuwa na mahali pa kukilaza kichwa Chake. Hiyo ni kweli. Alishuka sana, hata hakuwa na hat-. . .fukara sana, hata

hakuwa na kitanda cha kulalia. Yeye alisema, “Mbweha wana matundu, na ndege wana anga . . . wa angani, wana viota, bali Mwana wa Adamu hana hata mahali pa kulaza kichwa Chake.” Mnaona? Lakini Yeye alipata nini kwa ajili ya hayo? Aliinuliwa juu sana hata inambidi kuangalia chini apate kuiona mbingu.

142 Alikuja ulimwenguni, akachukua jina duni kuliko yote lililoweza kuchukuliwa ulimwenguni. Yeye alikuwa na jina duni kuliko yote, alichukua jina duni kuliko yote, akaitwa Beelizebuli. Beelizebuli ni . . . Walipomwona akizitambua roho kule namna hiyo, walisema, “Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni Beelizebuli, ibilisi.” Upiga ramli ni ibilisi. Nao walimwita Yeye ibilisi, duni kuliko wote. Yeye alikuwa na jina lililo duni kuliko yote.

143 Alienda kwenye mji ulio chini kuliko yote. Ndipo mtu aliye mdogo kuliko wote mjini akamwangalia akiwa juu Yake; Zakayo, hiyo—hiyo ni kweli, huko Yeriko. Huko chini kabisa, hakika alifanya hivyo. Alikuwa na jina lililo duni kuliko yote duniani. Alikuja duniani akiwa wa “haramu,” ndivyo walivyomwita, kwa sababu wao kweli wanaamini ya kwamba Mtoto huyo mchanga alizaliwa nje ya ndoa takatifu. Ilimbidi kukabiliana na hilo, kwanza kabisa. Kisha akaitwa jina la Beelizebuli, lililo duni kuliko yote lililoweza kupatikana. Yeye aliacha mahali Pake pa kimbinguni, akaja kuchukua hilo.

144 Lakini Mungu alimpa Jina lililo juu ya kila jina linalotajwa Mbinguni, kila jina linalotajwa duniani, hata jamii yote Mbinguni na duniani inaitwa Bwana Yesu. Haleluya! Jambo ndilo hilo. Aliacha; Yeye akapewa thawabu. Hakika, alipewa thawabu. Vema.

145 Alikuja duniani, Muumba wa mbingu na nchi, na Yeye hakuwa na chakula. Shetani alimjaribu, akifunga kwa ajili yetu, bali Yeye alipokea chakula ambacho wengine hawakujua chochote kukihusu.

Siku moja Yeye alisema hivyo. “Nina chakula.”

Kasema, “Mbona Wewe usije, ukale?”

146 Akasema, “Mimi ninacho Chakula msichokijua ninyi.” Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa na Chakula wasichojua chochote kukihusu.

147 Hapa duniani, Yeye hakuwa na kimbilio, wao walisema, hakuna mahali, hakuna nyumba, hakuna chochote alichomiliki Yeye. Lakini mnajua nini? Alifanyika Kimbilio kwa kila mmoja wetu. Mungu alimfanya Yeye Kimbilio, kwa ajili ya jamii yote ya binadamu. Hakuwa na kimbilio Lake mwenyewe, bali Yeye ndiye Kimbilio letu.

148 Wamekuwa wakizungumza sana juu ya makimbilio ya cheche za mnururisho. Loo, jamani! Tunalo moja. Hiyo ni kweli. Makimbilio ya cheche za mnururisho, kuingia kwenye shimo

fulani ardhini. Nao wananiambia, "Hayo mabomu yatapiga na kulipua shimo ardhini, futi mia moja na hamsini kwenda chini, kwa maili mia moja na kitu mraba." Mbona, ingevunja kila mfupa ndani yako, kama ulikuwa nusu maili huko chini ardhini. Hakika, ingeivunja, mahali popote. Bali tunalo Kimbilio. Kristo ndiye Kimbilio letu. Amina.

149 Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, wamekuwa, Urusi imekuwa ikijivunia majivuno yao makuu, hali, "Tumemweka mtu angani, wa kwanza."

150 Ninatofautiana na hilo. Tumekuwa na Mtu angani kwa miaka elfu mbili. Amina. Kweli. Naam, bwana. Mwombezi, naam, bwana, anayeenda Mbinguni na kurudi, katika . . . punde tu. Hakika. Tunaye Mtu angani. Wao hawana chochote. Naam, bwana. Kweli. Vema. Tunaona haikumbidi . . . Ilimbidi awe Kimbilio kwa ajili ya sisi sote.

151 Yeye aliuacha Uwana Wake, kati Yake na Baba, apate kufanyika dhambi kwa ajili yetu. Mlijua hilo? "Yeye hakujua dhambi; alifanyika dhambi kwa ajili yetu. Dhambi zetu ziliwekwa juu Yake." Yeye aliusalimisha Uwana, apate kuwa dhambi, sasa Yeye anaweza kuwafanya wenye dhambi kuwa wana. Amina. Hiyo ndiyo sehemu iliyo nzuri: kuwachukua wenye dhambi na kuwafanya wana, wakati Yeye alipousalimisha Uwana Wake apate kuwa dhambi, sasa Yeye huwachukua wenye dhambi na kufanya wana kutoka kwao. Amina. Ni majaliwa ya jinsi gani! Naam, bwana.

152 Mungu hawezi kulaghaiwa kwa chochote. La, bwana. Huwezi kufanya jambo hili, kwa sababu Mungu analishughulikia. Mwanawe alifanyika dhabihu ya dhambi, apate kununua sasa, kuwachukua wenye dhambi na kuwafanya wawe wana wa Mungu. Hilo ni jambo la kupendeza jinsi gani. Naam!

153 Sasa, naam, bwana, Yeye—Yeye alizitoa nguvu Zake. Akawa dhaifu, apate kuwa nguvu zetu. Yeye ndiye Nguvu zetu zinazotosheleza kwa yote. Hatuhitaji nguvu zingine zozote bali nguvu za Bwana Yesu. "Yeye ndiye Nguvu zangu siku kwa siku. Pasipo Yeye ningeanguka," kasema mshairi. Ajabu jinsi gani!

154 Yale unayoacha; yale unayopokea, kwa ajili ya yale uliyopata kuacha! Jamani! Uache ulimwengu. Yaache mawazo yako mwenyewe. Yaache mashaka yako. Yaache mahangaiko yako. Yaache, ukampokee Yeye. Mwamini Yeye.

155 Wasema, "Sasa, ndivyo ilivyo? Hivi siku za miujiza zimepita?" Achana na wazo la namna hiyo. Amini.

156 Mtu fulani alisema, "Kweli Yesu ni Mponya, ama hili ni lu—lundo tu la kusisimkwa kwa akili waliko nako watu hawa?" Liache tu wazo hilo, wakati mmoja.

157 "Sasa, unajuaje kama itakuwa ni kweli ama si kweli?" Ni ahadi. Hivyo ndivyo unavyojua.

158 Unasema, "Loo, ninaamini Roho Mtakatifu alikuwa ni kwa ajili ya watu huko nyuma kabisa, zamani za kale, kwa ajili ya wale wanafunzi tu." Loo, haiwezekani. Basi, kama ni hivyo, Biblia inajipinga yenyewe.

159 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Basi ni ahadi ya Mungu, kwamba tunaweza, wote wanaoitwa na Mungu kwenye Roho Mtakatifu, mna haki ya kuja. Yaache tu mawazo yako ya jambo Hilo, ulichukue Neno la Mungu lililokusudiwa kwa ajili yake.

160 Unasema, "Kuna kitu kama hicho, kwamba watu wanaweza kunena kwa lugha, ama huo ni ujinga fulani tu, ama kubwabwaja fulani wanakofanya?" Liache tu wazo lako mwenyewe.

161 Yesu alisema hivi, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Watanena kwa lugha mpya." Biblia ilisema hivyo. Naam, bwana.

162 "Ndugu, hizi ishara ninazoona mi—mikutanoni, hiyo inaweza ikawa ni Mungu?" Bila shaka, inaweza kuwa. "Vema, niliwaona watu walioishi maisha ya namna yoyote, nao wakaenda na kuwaombea wagonjwa, nao wakapata afya. Mimi . . . "

163 Yesu alisema, "Hakuna mtu anayeweza kufanya mwujiza katika Jina Langu, anayeweza kuninena Mimi vibaya moja kwa moja." Hiyo ni kweli.

164 Iwapo mtu huyo amekosea, kuichukua karama ya Mungu na kufanya jambo baya, Mungu atamshughulikia. Lakini ni Mungu, hata hivyo. Hakika, ndiye. Kwa sababu yeye ni mnafiki, inapaswa kukufanya wewe unawiri vizuri. Huwezi kuwa na . . . Njia pekee unayoweza kuwa na ninii halisi . . . Do—dola ya bandia, haina budi kufanyizwa kutokana na iliyo halisi.

165 Na kila mtu anasema, "Siendi kanisani. Sitaki kwenda kanisani. Kuna wanafiki wengi kupindukia." Mbona, wewe ni mdogo kuliko walivyo. Unajaribu kujificha nyuma yao. Ikiwa unaweza kwenda nyuma yao, wewe ni mdogo kuliko walivyo. Hiyo ni kweli.

166 Nilisoma makala ndogo gazetini hivi majuzi, ambapo mzee mmoja . . . Yeye alikuwa ni kiziwi, bubu, na kipofu, naye alienda kwenye shule ya Jumapili kila Jumapili. Nao wakamwuliza, kwa maandishi ya vipofu, kasema, "Mbona unaenda kanisani? Huwezi kusikia yale mhubiri aliyosema. Huwezi kusikia wowote wa hizo nyimbo. Kwa nini unaenda kanisani?"

167 Naye akasema, “Ninataka tu kumwacha kila mtu ajue niko upande gani.” Alitaka tu kumwacha ibilisi na kila mtu mwingine ajue yeye alikuwa upande gani. Nafikiri hilo ni zuri. Naam, bwana.

168 Yesu alifanya nini tena? Yeye aliyatoa na kuyaacha Maisha Yake mwenyewe. Aliyatoa Maisha Yake, apate kuyaokoa yako na yangu. Kwa sababu kwamba Yeye—kwamba Yeye aliutoa uhai Wake. . .Haikumbidi kuulaza chini. Aliulaza chini kwa hiari. Haikumlazimu kufanya hivyo, bali alifanya hivyo kwa hiari, kwa sababu Yeye angeweza kukuokoa. Na sasa Yeye ndiye pekee anayeweza kukuokoa. Hakuna kitu kingine kinachoweza kukuokoa.

169 Ninajua kuna dhehebu linalosema kwamba kanisa lao hukuokoa. “Unaokolewa na kanisa.”

170 Umeokolewa na Yesu Kristo la sivyo umepotea. Naam, bwana. Hakuna uwezalo kufanya, hakuna jambo moja uwezalo kufanya, ni kutubu tu dhambi zako. Yesu Kristo ndiye Mwokozi. Naam, bwana. Yeye alitoa, Yeye aliyatoa maisha Yake kwa ajili yako.

171 Sasa, nafikiri kwamba, leo hii. . .Tunapofunga, huenda tukasema hivi. Kwamba, inatupasa, basi, kwamba tungeyatoa maisha yetu na yote tuliyo nayo, na kuacha kila kitu kilicho cha kilimwengu, kila kitu kilicho kiovu, kutokuamini kwetu kwote, na kila kitu, tuweze kumfuata Yeye kama wale wanafunzi walivyofanya. Hivi hamngetaka kufanya hivyo? Kumfuata Yeye, kwa sababu gani? Kuona ishara Zake kuu za Kuja Kwake.

172 Sasa, kumbukeni, Biblia inaahidi, ya kwamba, katika siku hizi za mwisho, karibu tu na kumalizika kwa wakati, Nuru nyingine ya Kikristo itatokea. “Mvua ya masika na ya vuli zitakuja pamoja.” Nabii alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni. Kutakuwako na siku isiyoweza kuitwa mchana wala usiku.”

173 Hiyo ni siku ya namna gani? Kidogo ni ya mvua, yenye utusitusi, siku yenye ukiwa. Jua tu likiwaka, hakika, huko juu kabisa ya ukungu na mawingu kuna jua linalowaka. Na kupitia kwa hayo, ukungu huo wote, hata hivyo linatoa nuru, ili uweze kutembea, kuona jinsi ya kwenda huku na huku.

174 Hilo ndilo tumekuwa nalo kwa miaka na miaka, kwa miaka elfu mbili. Mnaona? Tumetembea kwa imani, nasi tumewazia, “Vema, hilo ni sawa. A-ha. Tunaamini, nasi tunajiunga na kanisa, na kuandika jina letu kwenye kitabu. Na hilo ni sawa. Tunaamini. Hatuyaoni mambo haya kama Yeye alivyofanya huko nyuma katika siku hizo, huko nyuma kabisa.” Wao walisema, “Yote hayo yamekwisha. Yamerudi.” Na imekuwa hivyo kwa—kwa mamia na mamia na mamia ya miaka, siku tu yenye utusitusi.

Ila Yeye alisema, “Katika wakati wa jioni, itakuwa Nuru.”

175 Sasa, jua lile lile linalochomoza Mashariki ndilo jua lile lile linalotua Magharibi. Yesu yule yule aliyekuwa . . . aliyeimwaga Roho Yake Mashariki, juu ya watu hao, ndiye Yesu yule yule aliye katika siku hizi za mwisho, akiimwaga Roho Yake, iko juu ya watu wa Magharibi. Yeye aliliahidi.

176 Yeye alifanya ahadi. Akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

177 Jinsi ambavyo Mungu alijidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa binadamu, akaketi hapo akala pamoja na Ibrahimu, huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, na kumwambia Sara yale aliyokuwa akiwazia, ndani ya hema. Akamwambia Ibrahimu jina lake lilikuwa ni nani, na jina la Sara lilikuwa ni nani, na jinsi ambavyo Yeye atakavyowazuru. Naye Sara hakuliamini, ndipo akacheka, ndani ya hema. Ndipo Malaika akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Ndani ya hema, nyuma ya huyo Mtu.

178 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku ile, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

179 Kama vile nimesema mara nyingi, nilivyosema jana usiku, ninataka kulinukuu tena. Daima kuna matabaka matatu ya watu, wakati wote, kama vile watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, wale wana watatu wa Nuhu. Kotekote chini, kuna—kuna matabaka matatu ya watu. Sasa sisi huwatambulisha hivi: asiyeamini, anayejifanya mwaminio, na mwaminio. Sasa hivyo ndivyo linavyoenenda. Lilifanya vile vile kule. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa kwenye hii."

180 Ibrahimu, ambaye alikuwa ameacha yote, apate kufuata, sasa hii hapa, moja kwa moja huku chini. Alikuwa ameishikilia hiyo ahadi kwa miaka na miaka, miaka ishirini na mitano. Huyu hapa, mwenye umri wa miaka mia moja sasa. Naye yuko hapa juu makondeni. Mifugo wake wanakonda, na hakuna maji. Naye, Lutu, akiishi kwa anasa huko chini pamoja na vitu vyote alivyotaka. Naye huyu hapa Sara, wakati mmoja alikuwa ndiye mwanamke mrembo kuliko wote nchini, na, huyu hapa sasa, kidogo amepungukiwa.

181 Na labda Bibi Lutu alikuwa na hii mitindo mipya ya kutengeneza nywele kichwa-maji wakati huo, mwajua, na upuuzi huu wote. Alikuwa akiishi tu kwa anasa huko chini. Alikuwa mke wa meya, naye alikuwa mfuasi wa kanisa lililokuwa ni kanisa kuu. Naam, bwana. Na hapana shaka alikuwa na mashirika yake yote. Hata hakutaka kuliishia, kuliacha, mpaka hata akaendelea kuangalia nyuma. Naye alikuwa amegeuka akawa nguzo ya chumvi kwa sababu alikuwa ameupenda ulimwengu kuliko alivyopenda kuitii sauti ya Malaika yule.

182 Sasa yaangalieni hayo matabaka matatu. Wasioamini, wale Wasodoma, wale wafuasi nusu tu wa kanisa, vuguvugu, walikuwa ni Lutu. Lakini wale wateule, kanisa lililoitwa litoke lilikuwa ni Ibrahimu na kundi lake. Wakati, Malaika hawa, walifika wapi? Kwa Ibrahimu na kundi lake. Kweli. Wakashuka, wawili wao wakashuka kule, kama wainjilisti mamboleo.

183 Tunao wainjilisti mashuhuri ambao—ambao wanaliendea kanisa la kimadhehebu siku hizi. Mmoja wa watu mashuhuri sana nchini, tumjuaye, ni Billy Graham. Naye bila shaka anawalipulia watu hao Injili huko nje, akiwaita watoke, "Tokeni Sodoma."

184 Haitupasi kupiga makelele "Tokeni Sodoma," kwa Kanisa hili. Linapaswa kuwa nje, tayari. Kama limeitwa na Roho Mtakatifu, tayari limetoka Sodoma, muda mrefu uliopita. Hiyo ni kweli. Limeiacha Sodoma. Linaishi huku nje, peke Yake, kabisa, limejitenga. Neno lenyewe *kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke, waliojitenga." Na kama umejitenga, ninii yako . . .

185 "Tokeni miongoni mwao. Msiguse vitu vyao vichafu." Kama hujafanya hilo, uko huko chini Sodoma; wewe ni mfuasi wa kanisa, vuguvugu. Basi unapaswa kujitenga, na kuyaondokea mambo ya ulimwengu, utoke, na kuishi maisha safi na matakatifu, ukatembee katika amri za Mungu.

186 Kumbuka, wawili wa hao Malaika walishuka kule. Hawakufanya miujiza mingi. Kunao mwujiza mmoja tu waliofanya, ulikuwa ni kuwapofusha hao watu walipowajia.

187 Vema, hivyo ndivyo hasa kuhubiriwa kwa Neno kunavyofanya, huwapofusha watu. Nao wainjilisti hawa mashuhuri siku hizi, tuwajuao, wengi wao huitembelea Phoenix hapa. Na—na wainjilisti mashuhuri kutoka . . . ambao wameingia hudumani, hawafanyi miujiza na kadhalika, bali kabisa wanawapofusha wasioamini, hao Wasodoma, kwa kulihubiri Neno, kwamba, "Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu."

188 Lakini, basi, hili hapa Kanisa la kiroho; sio kanisa la kawaida, wala Wasodoma. Lakini Kanisa la kiroho, wanaomwamini Mungu, wametembelewa na Mungu, kama Ibrahimu alivyotembelewa, huko chini kabisa. Ibrahimu ni mfano mkamilifu wa Uzao wa Ibrahimu baada yake, Kanisani, "Watu kutoka kwa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake," Uzao wa kifalme, kama nilivyohubiri Jumapili. Mnaona? Sasa, Kanisa hili, limeitwa litoke, likajitenga, likaacha kila kitu cha ulimwengu, likatoka, lipate kutembea pamoja na Roho Mtakatifu, kama Ibrahimu alivyofanya.

189 Tumeona kila namna ya mambo, kama Ibrahimu alivyofanya, akaja. Lakini ishara hiyo ya mwisho aliyoiona kabla ya mwisho wa safari yake ilikuwa ni ipi? Ishara ya mwisho ilikuwa nini kabla ya yule mwana aliyetarajiwa kuingia

jukwaani? Ibrahimu alikuwa akimtarajia mwana. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sisi ni Uzao wa Ibrahimu? ["Amina."] Basi tunamtarajia Mwana, Mwana aliyeahidiwa, Mwana wa Mungu.

190 Naye Ibrahimu aliziona kazi za ajabu za Mungu hapo Yeye alipomwita, kwenye ile Nuru ndogo wakati ule, na dhabihu, na kumthibitishia lile agano. Na mara nyingi Yeye alikutana naye kwa njia nyingi mbalimbali. Lakini ishara ya mwisho aliyomwonyesha Ibrahimu, ilikuwa ni wakati Yeye alipokuja, akidhihirishwa katika mwili, na kuketi huku ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema, na kumwambia Sara.

191 Ibrahimu hapana shaka aliamini kwamba huyo alikuwa ni Mungu. Baadhi ya watu hawaamini ilikuwa hivyo. Lakini, hiyo, Biblia ilisema alikuwa ni Mungu. Ibrahimu alisema alikuwa hivyo. Yeye alimwita Huyo, "Elohimu." Elohimu ni yule Muumba mkuu wa mbingu na nchi.

192 Sasa, Yeye alijifanyia Mwenyewe, mwili, kwa ajili ya ishara, kwamba katika siku za mwisho (Mnawaona hao Wasodoma, wasioamini? Mnamwona mfuasi wa kanisa?), sasa, angalieni wale Wateule, walioitwa watoke, na Yeye, katika huyu Mteule, Yeye anajidhihirisha Mwenyewe katika nguvu za Roho Mtakatifu, katika mwili wa binadamu. Amina. Hivi hamwezi kuona ni Masihi? Mungu, Kristo, aliyewakilishwa katika Kanisa Lake; Kanisa likifanya Maisha yale yale, likiishi maisha yale yale, likifanya ishara zile zile. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

193 Kama roho ya ja—jambazi ilikuwa ndani yangu, ningekuwa na bunduki. Kama roho ya mchoraji ilikuwa ndani yangu, ningechora picha ya mchoraji, na ningeweza kuchora. Kama roho ya makanika ilikuwa juu yangu, ningeweza kukwambia tatizo la gari lako. Unaona?

194 Basi kama Roho wa Yesu Kristo yuko ndani yangu, nitazitenda kazi za Kristo, kwa sababu ni Uhai wa Kristo ndani yako. Mnaona? Kudhihirishwa ndani ya Nani? Kumdhihirisha Nani? Yeye kuwa. . . Akauacha Uwana Wake, kisha akawa dhambi, na kuzichukua dhambi zetu, ili Yeye aweze kuwachukua wenye dhambi na kuwafanya wana. Alifanyika mimi, nipate kufanyika Yeye. Alifanyika mwenye dhambi, ili nipate kufanyika mwana wa Mungu. Yeye. . . Loo, ni—ni ajabu sana, yale Yeye aliyofanya. Mnaona? Yeye alipachukua mahali pako, ili uweze kupachukua mahali Pake. "Ninyi ni warithi pamoja na Yeye; katika Ufalme." Yeye alifanyika mwenye dhambi, kama wewe; dhambi zako zikawekwa juu Yake, ili Yeye aweze kukuchukua na kukufanya raia mwenza wa Mbinguni, na kukuweka pamoja na Yeye katika Ufalme wa Mungu. Haya basi: akaweka Roho Wake ndani yako. Basi kama Roho Wake yuko ndani yako, kazi alizozifanya Yeye wewe nawe utazifanya.

195 Sasa, angalieni yale Yeye aliyofanya wakati alipokuwa hapa duniani. Yeye alijitambulishaje?

196 Huwezi kukwepa, kuning'inia huku, na kwenda kwenye vyumba vya kamari, na kukaa mbali na kanisa, na kukaa nyumbani Jumatano usiku, kuangalia namna fulani ya mchezo mchafu wa televisheni, ama kitu kama hicho, na kuliacha kanisa lako, na yote namna hiyo, na kamwe utarajie kumwona Kristo. Huna budi kuyaacha mambo hayo yote, upate kumfuata Roho Mtakatifu.

197 Acha Yeye ajidhihirishe Mwenyewe kama Masihi, kama wale wafuasi wa kwanza walivyofanya. Walimfuata Yeye, kuona kama Yeye alikuwa ni Masihi. Unafikiri ilikuwaje wakati Andrea alikaa usiku kucha pamoja na Yeye usiku ule, yeye na Filipo? Kesho yake asubuhi, Filipo alipitia njia moja, naye Andrea nyingine.

198 Andrea akaenda kumtafuta ndugu yake. Na mara alipompata Simoni, yeye alisema, "Njoo, uone. Tumempata yule Masihi." Alijua Yeye alikuwa ni Masihi. Kwa nini? Alijua kile Masihi angekuwa. Alijua, Kimaandiko, kile Masihi angekuwa.

199 Sasa, hakika, Wayahudi, siku hizo, walikuwa wameyawazia yote, hayo makanisa makubwa mno. "Loo, Masihi atakapokuja, kutakuwako na baragumu itakayolia kote angani, kisha Mungu atauzungusha mpini fulani, na kuachilia ushoroba wa Mbinguni ushuke chini. Kisha kutakuwako na gwaride la Malaika litakalotokea kote duniani. Naye Masihi atakuja, akiendesha kupitia kwenye huo ushoroba namna hiyo, pamoja na Malaika na bendi, na mambo kama hayo, ashuke moja kwa moja kwenye hekalu *hili*, aingie ndani yake. Yeye atakuwa ni Masihi. Atachukua fimbo, na kuitawala dunia."

200 Tazameni jinsi alivyokuja vinginevyo, lakini Yeye kweli alikuja Kimaandiko. "Ameketi juu ya mtoto wa nyumbu, akaja, akaingia Yerusalemu, mnyenyekevu na mpole." Hiyo ni kweli. Mnaona?

201 Hilo hata lilimzungusha nabii, Yohana. Yeye alikuwa amemhubiri Masihi mwenye vipepeto mkononi Mwake, akiusafisha sana uwanda Wake; na Yeye alipokuja, mnyenyekevu na mpole. Lakini Yohana alijua huyo alikuwa ni Masihi, kwa sababu aliiona ile Nuru juu Yake. Naye alijua hivyo. Akasema, "Yeye aliyeniambia huko nyikani, 'Nenda, ukabatize kwa maji,' alisema, 'Yule utakayemwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, Huyo ndiye anayebatiza kwa Roho Mtakatifu na moto.'" Hakuna mtu mwingine aliyeiona. Yohana aliiona. Ahadi ilikuwa kwa Yohana.

Hakuna mtu aliyeiona ile nyota waliyoifuata wale mamajusi.

202 Na ndivyo ilivyo usiku wa leo. Unaweza kuketi hapa, kipofu maradufu, na usizione nguvu za Mungu. Usingeweza kulifahamu

mpaka Mungu afungue ninii yako . . . "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna mtu awezaye kuja isipokuwa Baba Yangu amemvuta." Hivyo tu. Hilo latosha.

203 Sasa tunaona ya kwamba waliacha yote, kisha wakamfuata Yeye na kuona kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Andrea alienda akamwambia Petro, kasema, "Unajua yale baba yetu aliyotwambia?" Kitu kama hiki, labda. "Tunajua ajapo Masihi, Musa alitwambia kwamba 'Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii' kama yeye tu. Nasi tunajua kwamba, tumefundishwa, 'Akiwepo mmoja kati yenu, aliye wa kiroho ama nabii, asemayo yakitimia, basi msikieni yeye. Yasipotimia, basi msimsikie.' Nasi tunajua ya kwamba Masihi atakuwa . . . sio tu nabii. Yeye atakuwa Mungu-Nabii. Kwa hiyo Mtu huyu ndiye Jamaa huyo."

"Unajuaje, Andrea?"

"Njoo tu, uone."

204 Akatembea kule. Ndipo mara alipoenda mbele za Yesu, Yesu alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni Mwana wa Yona." Alijua, papo hapo, huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

205 Huyu hapa Filipo anakuja, pamoja na Nathanaeli. Mara Nathanaeli alipomwendea, alijua . . .

206 Huenda wao, nadhani, mazungumzo makuu waliyokuwa nayo, wakizungumza habari zake, wakija huku. Na jinsi alivyokuwa amemwambia Petro mambo haya, na kumpa jina lingine, na kumwambia kwamba alikuwa ni nani, na baba yake, na kadhalika, juu yake. "Unajua Masihi anapaswa kuwa ni nabii."

207 Vema, huyu hapa anapanda juu basi, anaenda mbele za Yesu. Ndipo Yesu akasema, "Tazama Mwisraeli kwelikweli ambaye hamna hila ndani yake."

Akasema, "Rabi, ulinijua lini Wewe?"

208 Yeye akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

209 Akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli." Hilo lilitosha, kwake.

210 Maskini, mwanamke mwenye mashaka, mwovu, mchafu, akiishi na wanaume sita. Alikuwa ameolewa na watano, naye huyo aliyekuwa akiishi naye wakati huo hakuwa ni wake. Alitoka akaenda kisimani siku moja kuteka maji. Ndipo wakati alipoachilia pampu, ama ndoo kwenye winchi, chini, kuchota maji, basi alipoanza kuivuta juu, alimwona Mtu wa makamu ameketi pale, Myahudi. Kasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

211 Akasema, "Tuna ubaguzi. Hakuna—hakuna . . . sio desturi hapa Kwako, ukiwa ni Myahudi, kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho. Hatuna uhusiano."

212 Yeye akasema, "Lakini kama ulijua ni Nani aliyekuwa akizungumza nawe, ungeniomba Mimi maji unywe. Ungeniomba Mimi maji." Walininii tu . . . Waliendelea, wakizungumza mmoja na mwingine, kwa kitambo kidogo. Yeye alikuwa akifanya nini? Akijaribu kujua mahali shida yake ilipokuwa.

Sasa, "Yesu alikuwa na haja kupitia Samaria."

213 Kumbukeni, Yeye alijitambulisha tu pamoja na Wayahudi na Wamataifa . . . Hao ni watu wa Hamu, Shem. Mnaona? Watu wa Yafethi waliachwa. Sisi Waanglo-Saksoni, tulikuwa makafiri, tukiziabudu sanamu katika siku hizo. Kumbukeni. Kwa nini Yeye hakujitambulisha Mwenyewe, Yesu, hapo alipokuwa duniani, kwa Mataifa, katika ishara iyo hiyo, kuwaonyesha? Kwa sababu Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote.

214 Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi, nao Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi.

215 Naye akajidhihirisha Mwenyewe kama Masihi, katika kumwambia Petro, yule Yeye aliyempa funguo za Ufalme. Na kwa Nathanaeli. Naye Bartimayo kipofu, wakati imani yake ilipomsimamisha Yeye. Pia yule mwanamke aliyetokwa na damu. Na kadhalika, kwa Wayahudi.

216 Lakini Huyu hapa mbele ya Wasamaria, na Yeye akawajia Wasamaria, kujitambulisha Mwenyewe kama Masihi wa kweli.

217 Sasa, kwa mamia ya miaka, Wayahudi na Wasamaria pia waliamini Masihi alikuwa yuaja. Kwa hiyo, endapo Masihi alikuwa duniani, ni juu ya Masihi kujidhihirisha Mwenyewe.

218 Mwangalieni mzee Simioni hekaluni, akiwa na ushuhuda, ya kwamba, "Sitaona mauti mpaka nitakapomwona Kristo wa Bwana." Ndipo wakati ule ule ambao Mariamu alimleta Mtoto mchanga, Roho Mtakatifu alinena na Simioni. Akaenda moja kwa moja mpaka mahali alipokuwa, namna *hiyo*, kisha akainua mikono yake, na kusema, "Ruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani sawasawa na Maneno Yako, kwa kuwa macho yangu yanauona Wokovu Wako." Simioni asingeweza kuishi muda mrefu kutosha kumwona Yeye akitenda kazi Zake za Kimasihi, bali alikuwa na kumbukumbu kwamba Yeye alikuwa hivyo.

219 Lakini Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwa watu, kama Masihi, kuwa ni yule Mungu-Nabii. Mwanamke huyo, wakati alipozungumza naye, alisema, "Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

220 Kasema, "Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

221 Akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Tunajua, ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya. Hii itakuwa ndiyo ishara ya Masihi atakapokuja. Yeye Ndiye atakayetwambia mambo haya."

Ndipo Yesu akasema, "Mimi Ndiye ninayezungumza nawe."

222 Upesi akauacha mtungi huo wa maji akakimbia mjini, na kuwaambia watu humo mjini, "Njoni, mwone Mtu, Yule aliyeniambia yale niliyotenda. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hiyo si ndiyo ile ishara Masihi aliyokuwa atuonyeshe?"

223 Yeye kamwe hakuifanya mara nyingine tena, mbele ya yeyote wao, bali walisema watu wa mji huo walimwamini Yeye kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Amina.

224 Sasa ni wakati wa Mataifa. Tumekuwa na miaka elfu mbili ya vurugu, juu chini, madhehebu, ndani na nje, na mizozo na mabishano, na ugomvi na vita, na kila kitu kingine, wanathiolojia na seminari, na chochote zaidi.

225 Sasa, kama Yeye akiwaachilia hao Wasamaria na Wayahudi washuke moja kwa moja, waliokuwa wameiacha miungu ya ulimwengu, wapate kumtumikia Mungu, wakimtazamia Masihi ajaye, naye Masihi akajitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi kwa njia hiyo, katika siku hizo. . . Na Yeye hawezi kuzivunja kanuni Zake. Yeye siye Baba ambaye angefanya moja kwa mmoja, na mwingine kitu kingine, jambo lingine. Yeye ni Yesu yeye yule. Kweli.

226 Sasa, hapa, tumekuwa na miaka elfu mbili. Roho Mtakatifu ametushukia. Tulinena kwa lugha, na kuona ishara na maajabu, na kadhalika. Sasa, ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliona, kabla ya kurudi kwa mwana aliyeahidiwa, ilikuwa ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika mwili ambao ungeweza kula, kwa kubashiri na kuonyesha ishara ile ile ambayo Yesu alionyesha wakati alipokuwa hapa, kwamba ni Masihi. Sasa, Yesu alitabiri na kusema ingekuwa hivyo. Na, enyi marafiki, sasa saa imewadia.

227 Wayahudi hao waliosimama pale, wakati walipomwona Yesu akimwambia mtu huyo hivyo, wao walisema. . . Iliwabidi kulijibu kusanyiko lao. Wao, wao walijua lilitendeka, kwa hiyo wasingeweza kufanya lolote kulihusu. Iliwabidi kulijibu kusanyiko lao, kwa hiyo walisema, "Mtu huyu ni Beelizebuli. Yeye. . ." Waliwazia hilo moyoni mwao. "Mtu huyu ni Beelizebuli, mnaona, kwa sababu Yeye ni mpiga ramli, namna fulani ya mwa—mwanatelepathia, ama kitu fulani. Yeye ni Beelizebuli."

228 Yesu akayajua mawazo yao. Ndipo akawageukia, na Yeye akasema, "Mkisema hilo dhidi Yangu, Mwana wa Adamu, nitawasamehe. Bali, vinginevyo, siku moja Roho Mtakatifu yuaja, kufanya jambo lile lile. Basi kusema neno dhidi Yake, hakuna msamaha katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao."

229 Loo, ndugu, nina furaha sana usiku wa leo kuwa na baraka za kipentekoste. Amina. Hapana shaka ila hapa ndani, ndugu zangu, mmeketi humu ndani kutoka kwa Church of God,

Foursquare, Assemblies of God, na yote mbalimbali. Hilo ni zuri sana. Hilo, linaendelea tu kwenda. Msininii. . .Dumuni tu moja kwa moja nalo. Mnaona? Bali kamwe msiwazie ya kwamba hiyo blanketi haienei kwa ndugu yako mwingine, pia, katika dhehebu lingine ambalo (kadiri tu) lina Roho Mtakatifu vivyo hivyo. "Mungu aliwapa hao Roho Mtakatifu ambao walimtii Yeye." Kwa hiyo huyo ndugu mwingine alimtii, pia, mnaona, kwa hiyo itandaze tu upande huo mwingine. Hilo ni sawa. Na hebu tuje pamoja na kushangilia.

230 Tumeuacha ulimwengu. Sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Sisi ni Uzao wa Kristo, Uzao ulioahidiwa. Nasi hapa, papa hapa chini. Basi kitu cha mwisho kilikuwa ni kipi sasa, alichompa baba yetu Ibrahimu? Ishara ile, kabla ya Sodoma, kabla ya kule kuteketezwa kwa moto, na kule kuja kwa yule mwana. Sasa, kabla tu ya kule kuja kwa Mwana aliyeahidiwa, na kule kuteketezwa kwa Sodoma, Mungu aliahidi kupitia Yesu Kristo ya kwamba ingekuwa vivyo hivyo hasa, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma."

231 Angalieni ulimwenguni siku hizi. Historia ya ulimwengu haijapata kuona wapotovu wengi sana kadiri tulio nao siku hizi. Nazo barua zangu zimejaa akina mama, wakilia, kutoka hapa California. Tukisoma gazeti, kwamba upotovu, mbona, umebadilika katika California, nafikiri, yapata asilimia thelathini, kupita mwaka uliotangulia. Upotovu, uko kila mahali, uchafu. Shule, shule za kidini, zimelazimika kuwafukuza watu kutoka shuleni mwao, zina wakati mgumu kuwachagua. Wapotovu, "wakibadili matumizi ya asili," kama vile tu ilivyokuwa katika Sodoma, tunaliona hivyo.

232 Mwangalie Billy Graham, mjumbe kutoka kwa Mungu, huko chini, akieneza Injili hiyo.

233 Sasa, vipi kuhusu Kanisa, Teule? Linapaswa kuwa na ishara, pia. Hiyo si ni kweli? Linapaswa kuwa nayo. Ninatumaini usiku wa leo ya kwamba tutaachana na kutokuamini kwetu kwote, na kumwamini Bwana Yesu, na kumfuata, na kuziona ishara Zake za siku ya mwisho, kwa kuwa Yeye aliahidi zitakuwa hapa.

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

234 Kunaye mmoja hapa ndani usiku wa leo usiyemjua Yeye kama Mwokozi wako, nawe ungetaka kuacha kila kitu sasa hivi na kumfuata Yeye? Naomba uinue tu mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham. Ningetaka kufanya hivyo, kuwa Mkristo halisi." Mungu akubariki. Kunaye mwingine? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, na wewe, ndugu. Mwingine? Mungu akubariki, bwana. "Ningetaka kuacha kila kitu. Ni—nitafanya hilo, Ndugu Branham."

235 Ninataka kuuliza jambo fulani. Ndugu, dada, si—si—simaanishi kumwudhi mtu yeyote. Lakini, unaona, wewe—

wewe—wewe. . . Unawajibika kwa Neno. "Mki—mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu." Wakati mwingine inanibidi kusema mambo yanayonikatakata, hasa sana wakati mwingine kwa dada zangu.

236 Maana, mnatambua ya kwamba mwanamke ndiye Shetani alimtumia hapo mwanzo. Mungu alimchagua mwanamume. Shetani akamchagua mwanamke.

237 Alibarikiwa, hakika, kuwa kiangulio ambacho kilimleta Yesu Kristo duniani. Sasa, Huyo hakuwa Mwana wake. Nyote mnajua hilo. Yesu hakuna wakati mmoja alipomwita mama. Kamwe hakuwa na . . . Ni kusanyiko lililochanganyikana, bali nisikilizeni. Hapakuwapo na shahamu zilizotoka kwa Mariamu. Kwa Jumla ziliumbwa, bikira, na Mungu. "Roho Mtakatifu alitia uvuli." Hiyo ndiyo sababu Yesu asingeweza kumwita mama. Yeye hakuwa ni sehemu yake, hakuna kitu. Yeye alikuwa tu ni kiangulio ambacho Mungu alitumia, kumleta Mtoto huyo.

238 Maana, kama kungalikuwako na chochote cha mwanamke huyo kilichokuwa cha Mvulana huyo, Mtoto huyo, mwanamke huyo (mnaelewa; ninyi watu wazima mnajua ninalomaanisha), ilibidi kuwe na utiaji mimba wa namna fulani, namna fulani ya shahamu itoke kwa mwanamke huyo, kupitia hilo, basi ilikuwa kabisa ni kama tendo la kujuana kimwili pamoja na Mwenyezi Mungu. Isingewezekana.

239 Mungu alimwumba huyo mtoto, yai na Damu pia. Seli zote mbili, za mwanamke na za mwanamume, Mungu aliziumba. Hiyo ndiyo sababu mwili huo ulifufuliwa. Bila shaka. Yeye alikuwa ndiye wa kwanza wa ufufuo. Kwa hiyo Yeye kamwe hakumwita mama. Wao walisema, "Mama yako yuko hapa nje akikutafuta Wewe."

240 Yeye akasema, "Mama Yangu ni nani?" Kasema, "Hao wafanyao mapenzi ya Baba Yangu, hao ndio mama Yangu." Mnaona? Kwa hiyo Yeye hakuwahi hata wakati mmoja kumwita mama. Alimwita "mwanamke." Hivyo ndivyo alivyokuwa.

241 Na baadhi yenu Wakatoliki wapendwa mnamfanya yeye mungu, ama mungu mke, malkia wa Mbinguni. Si sahihi. La, sivyo. Yeye alikuwa ni mwanamke mzuri. Naam, bwana. Kweli kabisa. Bali yeye hakuwa ni zaidi ya mwanamke yeyote mwingine ambaye Mungu anachagua kumtumia. Anaweza kumtumia mwanamke kwa jambo lingine. Anaweza kumtumia, kwa njia yoyote. Yeye alikuwa ni kiangulio tu, kwa sababu hivyo ndivyo alivyokuwa, apate kuipa hiyo Mbegu joto, na kadhalika namna hiyo. Nao Uhai uliingia katika Mtoto huyo mchanga. Ila Damu, himoglobini, daima tunajua, hutoka kwenye jinsia ya kiume. Na Yeye alikuwa ndiye wa kiume, Muumba. Mwanamke hakuwa Myahudi wala . . . Huyo Mtoto alikuwa . . .

242 Yesu hakuwa Myahudi wala Mmataifa. Yeye alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kweli. Mungu alijiumbia Mwenyewe mwili

ambao Yeye aliishi ndani yake. Huyo alikuwa ni Mwana Wake, Yesu Kristo. Huo uzazi mtakatifu, wa kibikira ulimzaa mwanadamu huyu, kuchukuliwa mimba kwa Roho Mtakatifu pasipo na ile dhambi ya asili. Mwanamke hakuwa na uhusiano wowote nalo, si yai wala chembe ya damu.

243 Mwanamume ana chembe ya damu. Mwanamke analo yai. Kwa njia hii, ingebidi kuwe na namna fulani ya tamaa na kutiwa mimba, kusababisha jambo fulani kutukia.

244 Basi kwa kisa hicho, hakukuwako na kitu ila kutiwa uvuli kwa Roho Mtakatifu, naye Mungu akaumba ndani ya huyo mwanamke. Huyo ndiye Mwokozi wangu. Bila Yeye, sote tumekwisha.

245 Sasa, baadhi yenu watu hapa, ninyi wanawake, ninyi, labda wanawake wa Kipentekoste, mmekuwa na hatia ya kuvaa nguo za kizinifu, kukata nywele zenu, kufanya mambo. Nimeona hapa California, hamna wengi mno wa hao . . .

246 Ama, hapa Arizona, hasa, sio wengi mno wanaojipodoa. Hilo lilipigwa vita, pia. Vema, hakuna kitu katika Biblia cha kusema usijipodoe. Tunajua tu kwamba ni vibaya, maana ni kwa ulimwengu.

247 Ila kunayo amri katika Biblia ya kwamba mwanamke, anayezikata nywele zake, ni mtu asiye na heshima. Na kama linaonekana hivyo kwa Mungu, nanyi mnasema mnaye Roho Mtakatifu, na kufanya hivyo, kuna kasoro fulani.

248 "Kuvaa vazi limpasalo mwanamume." Loo, dada, mpendwa, usijifananishe na ulimwengu. Uache ulimwengu. Shikilia kwa Kristo.

Unasema, "Inaleta tofauti gani?"

249 "Heri ni yeye anayezifanya amri Zake zote, apate haki ya kuingia kwenye ule Mti wa Uzima." "Mwenye hatia katika madogo sana ana hatia ya yote."

250 Unajua vema zaidi. Ukimpokea Roho Mtakatifu, hakika Yeye atakwambia vizuri zaidi. Atakwambia vizuri zaidi, kama ni Roho Mtakatifu.

251 Sasa, kama una hatia, nawe ungetaka kuanza upya usiku wa leo, na kusema, "Ndugu Branham, sikutambua hilo. Nimekuwa nikitelezateleza. Ninataka kuanza upya. Tangu sasa na kuendelea, nitamtumikia Mungu." Inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Mungu awabariki. Hilo linahitaji ujasiri. Hilo linahitaji ninii halisi . . . Mungu awabariki. Mikono mingi. Vema. Mungu awabariki. Halafu, kama unajua, ya kwamba Kitu fulani ndani yako, kinakwambia umekosea, basi unajua Mungu yuko karibu nawe.

252 Lakini unapolisikia Neno dhahiri sana, na halafu ungali unaketi hapo na kusema, "Sitafanya hivyo. Yeye hajui analozungumzia," nami huku nikilinukuu Neno papa hapa,

unaona, basi kuna kasoro na kile kilicho ndani yako. Unaona? Si kitu ila kimoja, ni Shetani. Hivyo tu. Ni kumpinga Mungu. Ni kukiuka kanuni Zake. Ni dhidi ya Neno Lake.

253 Mtu fulani aliniambia, sio muda mrefu uliopita, mhubiri mashuhuri. Akasema, "Ndugu Branham." Akaniita chumbani mwake, akaweka mikono yake juu yangu. Kasema, "Wewe utaiharibu huduma yako."

Nikasema, "Ati nini?"

254 Kasema, "Sikuzote unawakemea watu, jinsi wanavyotenda." Kasema, "Mbona usininii . . . watu wanafikiri wewe ni nabii."

Nikasema, "Mimi si nabii."

255 Akasema, "Vema, watu wanafikiri ndivyo ulivyo. Kwa nini usiwafundishe mambo ya kiroho, jinsi wanavyoweza kupokea baraka kuu za kiroho na kadhalika?"

256 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha mambo ya kiroho wakati hata hawajui ABC zao? Hata hawatakuwa na adabu za kawaida kujiweka sawa na Neno, acha mambo ya kiroho. Ikiwa hawayaamini mambo ya duniani, watayaaminije mambo ya kimbinguni?"

Akasema, "Vema, wewe utaiangamiza tu huduma yako."

257 Nikasema, "Huduma yoyote ambayo Neno la Mungu litaangamiza, inapaswa kuangamizwa." Rudini kwenye Neno. Hiyo ni kweli.

258 Sasa, kama unavuta sigara, na kadhalika namna hiyo, na kudai unaye Roho Mtakatifu, aibu kwako. Ninyi wanaume! Mnasema, "Kwa nini unawaonea wanawake?" Ninyi wanaume mtakaowaacha wake zenu wafanye hivyo, loo, bwana, unayejiita Mkristo, aibu kwako.

259 Ninajua hili ni kali. Lakini, ndugu, ni—ni wakati wa kujiweka tayari. Ni wakati wa Roho Mtakatifu kuja, kumchukua Bibi-arusi Wake. Na endapo hatajiweka sawa na Neno Lake, basi kuna kasoro.

260 Ninyi ambao mmeanguka, mnaokaa nyumbani Jumatano usiku wala hamtakuja hapa kanisani, mkiziangalia televisheni, na siku zingine usiku za kanisa! Wazieni, hakika m—mnasema, na kama inawabidi kuja kanisani, inakubidi kujilazimisha kuja, kwa sababu unafikiri ni sheria kufanya hivyo. Unapaswa kufanya hivyo. Ni vizuri kufanya hivyo. Na kama hupendi kufanya hivyo, kuna kasoro. Yupo Roho Mtakatifu anayekufanya kupenda kumtumikia Mungu.

261 Sasa, pamoja na hayo, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, wote wanaojisikia ya kwamba wangetaka kuanza kwa Mungu, usiku wa leo, inua mkono wako. Ni kila mtu tu hapa sasa, inua tu mkono wako, kila mtu, kote. Mungu akubariki, akubariki, wewe, wewe, wewe, wewe. Mungu awabariki. Sawa. Nitawaombea.

262 Baba wa Mbinguni, sasa nimenena Maneno Yako kwa udhahiri na waziwazi, na kukata, kadiri nijuavyo. Sio niwe tofauti; kama hilo lingekuwa ndilo msimamo wangu, Bwana, ningepaswa niwe ndiye niliye madhabahuni. Lakini kama nikimwona mtu fulani, ndugu yangu ama dada, akizama katika maskini mtumbwi mchakavu unaovuja, wala nisiwapigie makelele, ama kuwakemea, ama kwa namna fulani niwatoe kwenye janga hilo, basi siwapendi. Ninajaribu kuwatoa, Bwana, ili waweze kuwa salama.

263 Ee Mungu wa Mbinguni, ninamwombea kila mmoja walioinua mikono yao. Nimeona wengi wa hao maskini wanawake waliokata nywele zao wakiinua mikono yao, wakiwa na neema ya kutosha hata wanajua ya kwamba wamekosea. Kulikuwa na wengine ambao hawakufanya hivyo. Sasa, Wewe ndiwe Hakimu wa hilo. Lakini ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utawaokoa hao. Lijalie. Kamwe . . .

264 Hao wanaume waliinua mkono wao, vijana wanaume wazuri sana wanaoketi pamoja na wake zao, na kadhalika, waliinua mkono wao. Wazee waliinua mikono yao. Sasa, Baba, hatuna budi kuuacha ulimwengu na mambo ya ulimwengu, la sivyo hatuwezi kukutumikia Wewe.

265 Ninaomba ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe usiku wa leo katika njia ambayo watu wataona, ya kwamba, Neno ambalo limenenwa. Watu wanaweza kusema lolote. Lakini wakati Mungu anapokuja huku na kulithibitisha Neno Lake, anathibitisha kwamba ni Neno Lake, basi tunaachwa wakati huo bila udhuru wowote. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utalijalia usiku wa leo. Na mara watu hawa . . .

266 Labda wengi wao ni wenye dhambi. Wengi waliinua mikono yao, kama wenye dhambi. Nami ninaomba, Baba, mara watakapoona madhihirisho . . . Na kutumaini ya kwamba Wewe utafanya hivyo usiku wa leo, utajionyesha Mwenyewe, kwamba mwisho umewadia. Yule Mwana aliyetarajiwa atawasili hivi karibuni kwa Uzao wa Ibrahimu, na kwamba Sodoma itateketezwa kwa moto.

267 Siku moja hapatakuwapo na jiwe lililosalia juu ya lingine, la Phoenix. Hili bonde litafagiliwa kabisa. Humu mjini usiku wa leo ambako kuna uzinzi, unywaji wa pombe kali ya mseto, akina mama wanaovuta sigara, mabinti, kucheza dansi, kujinengua, kupiga makelele, wanaume wakiishi kizinifu, dhambi ya mji huu! Ee Mungu, lakini ninaangalia chini kupitia kwake, na kuwazia, "Kuna haja gani hata kujaribu?"

268 Lakini basi ninaangalia chini kupitia kule na kuona Nuru ndogo *hapa* na *pale*, Mkristo aliyejiweka wakfu, akiomba. "Wote wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yanayofanyika kati ya mji, Malaika aliagizwa kuweka Muhuri juu yao, kuwatia alama, nao ndio ambao hawangeangamizwa." Nami ninaomba,

Baba, kutakuwako na wengi watakaokuwa Mkristo aliyejiweka wakfu, amehusika sana, haogopi kuukemea uovu. Mungu, katika siku hizi, jalia tuzungumze mambo yaliyo sahihi.

269 Na kutakuwako na Siku ya Hukumu itakayokuja, ndipo basi hawatakuwa na udhuru, kwa kuwa Ujumbe huu usiku wa leo utarushwa kwenye skrini, kanopi za mbingu, nasi sote tutajibu. Kwa hiyo ninaomba, Baba, kwamba Wewe utaitahiri mioyo yao na mambo yoyote ya ulimwengu, ili waweze kuishi kitauwa katika ulimwengu huu wa sasa. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

270 Ninasikitika sana kuwaweka. Sisi. . . Ni—nimechelewa sana. Wala si—sininii. . . Ninapaswa kuwa nimetoka. Ninii ya mwisho. . . Kila usiku, nilitoka kwenye, yapata saa nne, tukichelewa sana. Nilitaka kutoka usiku wa leo saa tatu na nusu. Sikufanya hivyo.

Sasa, hebu kidogo tu, kutia mu—muhuri kwa yale nimesema.

271 Sasa, kweli, mimi si mhubiri. Mtu yeyote anajua hilo. Sina elimu, nami hutumia maskini maneno yangu ya Kentaki ya "yake," "aiko," na "dote," na "tafuta," na "beba," na "hao walo." Nanyi mwajua mimi si mhubiri namna hiyo. Sina elimu ya kuwa hivyo.

272 Lakini mimi ni Mkristo. Bwana Yesu aliniokoa na dhambi. Najua hilo. Na Yeye alinipa Neno lingine kuthibitisha machache niyajuayo. Jambo pekee, mimi sijaribu kuweka tafasiri yoyote ya kibinafsi. Ninalisoma tu. Na lolote Hilo lisemalo, mimi nasema jambo lile lile. Mnaona? Hayo ndiyo yote nijuayo. Mnaona? Sasa, kama limefasiriwa vibaya, sijui mimi. Ninalisema tu jinsi limefasiriwa *hapa*. Mnaona? Na Yeye sikuzote alidumu nyuma yake, na kuliunga mkono.

273 Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo yuaja hivi karibuni. Ninaamini kwamba Yeye ni Yesu yeye yule, jana, leo, na hata milele. Ninaamini ya kwamba Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu," kosmosi, utaratibu wa ulimwengu, "hautatuona tena. . . hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona Mimi, ninyi, Kanisa, kwa kuwa Mimi," kiwakilishi nafsi, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Mnaamini hilo? Tuliona ni kazi gani Yeye alizofanya, jinsi Yeye anavyojidhihirisha Mwenyewe.

274 Ninaomba, usiku wa leo, kwamba Mungu atalichukua kanisa hili. . . Sasa, haidhuru ni kiasi gani Yeye angenipaka mafuta, Yeye hana budi kuwapaka ninyi, pia. Mnaona? Haijalishi ni kiasi gani Roho Mtakatifu angejaribu kunena *hapa,* hana budi kuwa na kitu fulani *huko* nje, kumsikiliza.

275 Yesu alipitia kwenye kundi la watu, siku moja, nao walikuwa wakipaza sauti, "Rabi, Rabi, tuna furaha kuwa nawe hapa, *fulani-na-fulani*." Yesu akizidi tu kusonga mbele.

276 Na kulikuwako na maskini mwanamke aliyekuja hapo na kugusa upindo wa vazi Lake, ndipo akarudi akaketi chini. Yesu alisimama na kusema, "Ni nani aliyenigusa?"

277 Mbona, Simoni Petro akamwambia, kana kwamba, mbona, yeye alimkemea. Akasema, "Mbona, kwa nini Wewe useme jambo kama hilo? Kila mtu anakugusa."

278 Akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa mnyonge. Nguvu," ambazo ni uweza, "zimenitoka."

279 Akaangalia kote juu ya hilo kusanyiko. Kulikuwa na mtu fulani aliyemwamini. Haidhuru, huenda kulikuwako na mamia pale, bali palikuwapo na mtu aliyeamini. Akampata maskini mwanamke huyo, akamwambia juu ya kutokwa kwake na damu, kulikuwa kumekoma, naye akaponywa. Hiyo ni kweli? Akaendelea mbele. Mnaona? Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

280 Sasa, tumezisambaza kadi za maombi. Tulisambaza nusu yake, huko jana usiku, nusu yake usiku wa leo.

281 Hivi tulianza kutoka ya kwanza, jana usiku? Tulianza na za kwanza kumi na tano ama ishirini, jana usiku, kutoka moja hadi *fulani-fulani*? Ati nini? Wasemaje? [Ndugu fulani anasema, "Ishirini."—Mh.] Moja hadi ishirini. Vema. Wengi wao wako hapa usiku wa leo.

282 Hebu tutoe zingine kutoka nyuma yake, basi. Hebu tuanze. Hebu tuone. Tunazo dakika kumi na tano, hebu tuwape kadi kumi na tano, basi. Hebu tuone, hiyo ingekuwa ni themanini na tano hadi mia moja. Hebu tuanzie kwenye themanini na tano, hadi mia moja.

283 Ni nani aliye na kadi ya maombi themanini na tano? Inua mkono wako. Themanini na tano, mwanamke huko nyuma? Njoo hapa, dada. Themanini na sita, ni nani aliye na themanini na sita? Papa hapa. Themanini na saba, themanini na saba. Mtu fulani inua mkono wako, themanini na saba. Mtu huyu, themanini na saba. Themanini na nane, themanini na nane. Themanini na tisa, themanini na tisa. Tisini, tisini na moja, tisini na mbili, tisini na tatu, tisini na nne, tisini na tano, tisini na tano. Naam. Tisini na sita, tisini na saba. Tisini na sita, sikuiona ikiinuliwa, tisini na sita. Sasa, kama unayo kadi yako, njoo. Mnaona? Tisini na saba, tisini na nane, tisini na tisa, mia moja. Vema. Wakati watu hawa. . . Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa. Kuna yapata wanane waliokosekana.

284 Sasa sikilizeni. Ni kweli. Usije hapa juu na dhambi ikining'inia maishani mwako. Afadhali uikiri ukiwa huko nje, kwa Mungu. Lakini kama—kama unayo, kama umekiri dhambi yako, njoo huku.

285 Ni wangapi huko nje wasio na kadi ya maombi, nawe unataka Yesu akuponye? Inua mkono wako. Ni wangapi

wangeamini, iwapo Yesu Kristo angefanya . . . Kama Yeye . . . Ni wangapi wanaoamini hili?

286 Angalieni. Nitawaomba wahudumu hawa walio nyuma yangu. Ndugu zangu, ni kweli, kama wahudumu wa Injili, tunaamini ya kwamba Biblia, Agano Jipya, Kitabu cha Waebrania, kinasema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Hiyo ni kweli, ndugu zangu?

287 Ni wangapi huko nje wanajua ya kwamba Biblia inasema hivyo? "Kuhani Mkuu."

288 Vema, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, sasa, Yeye alitendaje, kama ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, basi, Yeye alitendaje wakati mtu fulani alipomgusa na mambo ya udhaifu wao? Maskini yule mwanamke mwenye kutokwa na damu, ambaye alimgusa Yeye, kwa sababu alikuwa na haja ya kuguswa; Yeye aligeuka, akaangalia kote mpaka akampata, akamwita. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli, ndugu zangu? Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, itambidi Yeye kutenda vivyo hivyo, kwa sababu Yeye ni—Yeye ni Kuhani Mkuu. Hiyo ni kweli? Vema, itambidi Yeye kutenda vile vile.

289 Sasa, hamhitaji kadi za maombi. La. Huhitaji kadi ya maombi. Kitu pekee unachohitaji ni kumwamini Mungu. Kuwa na imani, amini tu kwa moyo wako wote ya kwamba Yesu Kristo huwaponya wagonjwa na wanaoteseka, na Yeye bila shaka atafanya hivyo.

290 Sasa, hebu tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi sasa, tena, kabla ya kusemwa au kufanywa chochote. Sasa, sisemi ya kwamba Yeye atalifanya. Ninatumaini ya kwamba atalifanya. Lakini na—naamini, na ninatumaini ya kwamba Yeye atalifanya. Sasa, kama Yeye atafanya hivyo, ni wangapi wenu wataamini? Inua mkono wako. Na alijalie, ndilo ombi langu.

291 Baba wa Mbinguni, sasa nimesema yale Neno Lako lisemayo, "Kuacha yote, kukufuata Wewe." Wale walioacha yote, walipata kukuona Wewe. Na haidhuru Wewe ungefanya nini, wale ambao hawataiacha dhambi na kufuata, kamwe hawataweza kuelewa. Wale wanaoiacha dhambi, kutokuamini . . .

292 Tunajua ya kwamba dhambi ni kutokuamini. Haijalishi jinsi tunavyoishi kitakatifu, yale yote tufanyayo, kama tungali hatuamini, sisi ni wenye dhambi. Biblia inasema, "Asiyeamini amehukumiwa tayari." Kwa hiyo tunajua ya kwamba hatuna budi kuamini "kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu." Hicho kinapaswa kuwa ndicho chakula chetu cha kila siku.

293 Nami naomba, Baba, ya kwamba, kama vile nimenukuu kutoka kwenye Maandiko usiku wa leo, Ahadi Zako za siku hizi za mwisho, na kile tunachopaswa kuangalia katika siku hizi za

mwisho. Kama hiyo imekuwa ni kweli, Bwana, basi yathibitishe Maneno haya kwa ishara zitakazofuata. Tujalie.

294 Ninajikabidhi mwenyewe Kwako, pamoja na Neno, na hawa watu. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utaitahiri mioyo huko nje, wapate kuamini kwa moyo wao wote, na hasa sana hawa watakaokuwa kwenye mstari wa maombi. Kisha uwajalie watu waone ya kwamba Masihi, Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, yupo pamoja nasi usiku wa leo. Yumo Kanisani, Kanisa Teule, lililoitwa litoke, Uzao wa Ibrahimu, kwa ahadi ya kifalme. Tujalie, katika Jina la Yesu. Amina.

295 Sasa, sasa hebu niangalie tu, kwa dakika moja. Sasa, tutachukua tu wakati wetu, kwa dakika chache tu, chache tu sana, kama dakika kumi.

296 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnamwamini? ["Amina."] Mnaamini vitu hivi ambavyo nimewasomea kutoka kwenye Neno usiku wa leo ni kweli? ["Amina."] Mnaamini Yesu alifanya hivyo wakati Yeye alipokuwa duniani? ["Amina."] Mnaamini Yeye aliliahidi? ["Amina."] Mnaamini tuko katika siku za mwisho? ["Amina."] Sasa, hiyo ni ahadi Yake. Hana budi kuiishi hiyo. "Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakalo. Mtatendewa." Sasa, nia na kusudi lako halina budi kuwa sahihi. Huna budi kuamini hilo kwa moyo wako wote.

297 Sasa, siamini ya kwamba kuna mtu kwenye mstari wa maombi ninayemfahamu. Hatufahamiani. Mimi ni mgeni. *Huko* nje, wageni. Nyinyi nyote mnaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, ninyi mlio kwenye mstari huu mdogo wa maombi *hapa*, inua mkono wako, unayejua sijui chochote kukuhusu. Vema. Wote *huko* nje, wanaojua ya kwamba sikujui, au sijui chochote kukuhusu, inua mkono wako, angalieni tu. Haya basi. Basi, ni jambo lililofichwa. Hawa *hapa* walio na kadi za maombi. Yule *pale* mmoja asiye na ninii ya maombi . . .

298 Kadi ya maombi si kitu ila kadi ndogo iliyo na namba juu yake. Inakupa tu namba, huyo mvulana hushuka anakuja na kuzichanganya, ndipo mtu yeyote anayetaka kadi ya maombi anaweza kupata. Wala yeye hajui, hakuna yeyote mwingine anayejua, ambapo mimi . . . Vema, yeye asingejua kama kadi zote zimechanganywa pamoja, kutoka mahali pamoja hadi pengine. Kamwe hawajui ni nani atakayekuwa kwenye mstari wa maombi, maana hatuwezi kujua hilo. Mara nyingi, tunazipeleka huko chini . . .

299 Nilipoanza kwa mara ya kwanza, tulimpata mtu mmoja huko chini akiziuza kadi za maombi. Mtu mmoja alisema, "Nitakupa dola mia tano kumweka mke wangu mstarini." Mnaona?

300 Nikamchukua mwanangu mwenyewe. Ndipo nikasema, "Mwanangu, ili kujiweka sawa kwa watu, kusudi wajue ya kwamba usingeuza kadi ya maombi, nenda mbele zao,

zichanganye kadi za maombi namna *hii,* kisha uzisambaze kwa mtu yeyote anayehitaji. Na mbali na hayo, mwanangu, kamwe hutajua mahali nitaanzia kuita mpaka nitakapofika huko."

301 Ni wangapi wameona hilo katika mkutano, wakati baada ya wakati? Kila wakati tu, nitabadilisha, na kwenda *hapa*, *pale*. Na halafu, mbali na hayo, ambapo mtu mmoja anaponywa jukwaani, kunao dazani moja wanaoitwa *huko* nje, mnaona, hiyo ni kweli, bila kadi za maombi.

302 Kwa hiyo ni kutokosea kwa Bwana Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

303 Utaacha yote, kumfuata Yeye? Uko tayari kuacha kutokuamini kwako, upate kumfuata Yeye kwa ajili ya uponyaji? Yaache mambo yako—yako ya ulimwengu, upate kumfuata Yeye katika utakatifu, na kumtendea Yeye kazi. Fanya hivyo sasa. Sisemi kwamba atalifanya. Akilifanya, basi utajua.

304 Mwanamke huyu anayesimama papa *hapa,* hii ni pi—picha tena, kama nilivyosema jana usiku, ya Yohana Mtakatifu 4. Hawa hapa mwanamume na mwanamke, wakikutana kwa mara ya kwanza maishani. Na ilikuwa kwenye benchi ndogo. Kama uliwahi kuwa huko Samaria, nje ya Sikari pale, kile—kile kisima kidogo, kuna mandhari ndogo, mizabibu kando yake, namna *hiyo*. Hapo ndipo huyo mwanamke alipoketi, akazungumza na Yesu. Mwanamume, mwanamke, walikutana kwa mara ya kwanza. Naye akamwambia mwanamke huyo shida yake ilikuwa ni nini. Shida yake ilikuwa, alikuwa mwenye dhambi.

305 Huenda ikawa ni yeye. Huenda akawa ni mwenye dhambi. Huenda akawa ni mnafiki. Huenda akawa ni mtakatifu. Huenda akataka uponyaji kwa ajili ya mwili wake. Huenda akataka uponyaji kwa ajili ya mtu mwingine. Huenda akawa na fedha. Yeye, sijui yupo hapa kwa sababu gani. Siwezi kuwaambia. Amesimama tu hapo, mwanamke. Hivyo tu. Hiyo ni kweli. Hatujawahi kukutana. Bali kama Bwana Yesu atakuja hapa . . .

306 Sasa, kumponya, ikiwa yeye ni mgonjwa, siwezi kufanya hivyo. Siwezi kufanya yale Mungu amefanya tayari. Sasa, jambo pekee . . .

307 Vipi kama Yesu alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii? Kama akija kwa Yesu na kusema, "Yesu, utaniponya?"

308 Vema, Yeye angesema, "Mtoto Wangu, tayari nimefanya hivyo. Nilijeruhiwa kwa makosa yako. Kwa kupigwa Kwangu uliponywa." Hiyo ni kweli? Ni kazi iliyomalizika.

309 Unakuja, unasema, "Yesu, utaniokoa? Utaniokoa?" Hilo silo swali. Yeye tayari amelifanya.

310 "Bwana Yesu, ninakubali Upatanisho Wako. Mimi ni mwenye dhambi." Mnaona? Uliokolewa huko nyuma. Uliponywa huko nyuma. Ndio kwanza uukubali. Kwa imani umeokoka. Kwa imani unaukubali wokovu wako.

311 Na mtu yeyote anayekuja huku, anawaambia wanazo nguvu za uponyaji, nao wanaweza kuwaponya, utakuwa . . . wewe achana na hayo kabisa, maana sivyo. Nguvu za uponyaji ziko katika Kristo, kazi iliyomalizika tayari.

312 Kama mtu akikwambia Mungu amempa uwezo kusamehe dhambi zako, na kufanya hivyo, usiliamini. Zimesamehewa tayari. Yesu akisimama hapa usiku wa leo, jambo pekee, ingetangaza kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu.

313 Vipi kama Yeye alikuwa . . . Vipi kama sasa mikono yangu ilikuwa imejaa makovu ya misumari, na damu ikitiririka kutoka kwake, na miiba kote *hapa*? Hiyo bado isingemfanya Yesu. Huo ungekuwa ni mwili wangu.

314 Nasi tunajua ya kwamba mwili huo umeketi mkono wa kuume wa Mungu. Nao utakapokuja, hapatakuwako na wakati baada ya hayo. Hiyo ni kweli. Yesu atakaposhuka, hakuna lingine.

315 Lakini Yeye yupo hapa katika mfano wa Roho. Halafu Uhai Wake uko ndani yako na ndani yangu, kukupa imani na kunipa imani.

316 Sasa, angalieni hapa. Hii—hii maikrofoni, kama hakukuwako na sauti hai hapa kuzungumza ndani yake, ingekuwa ni bubu kabisa. Hiyo ni kweli?

317 Sasa, angalieni. Sikilizeni kwa makini, kusudi msilikose sasa. Kisa hiki, iwapo Mungu atalifanya, atalitatua.

318 Sasa, maikrofoni hii haiwezi kuzungumza kamwe, kwa sababu haina kitu cha kuzungumzia. Hiyo ni kweli? Sasa, jinsi tu maikrofoni hii ingaliweza kuzungumza, ni kitu fulani kizungumze ndani yake.

319 Sasa, mimi huyu hapa. Simfahamu mwanamke huyo, kamwe sijawahi kumwona. Hiyo ni mikono yangu mbele za Mungu, naye aliinua mikono yake, kwamba hatukufahamiana. Sijui lolote kumhusu. Lakini, mpaka kitu Fulani kije *hapa* ndani, kusema kilicho shida *hapo*, mimi ni bubu, pia, maana sijui lolote. Mungu anajua hilo ni kweli. Mnaona? Inabidi kuwe na kitu Fulani kikizungumza.

320 Sasa, unaweza kufanya chaguo lako. Kama wewe, kama vile Filipo, yeye alisema . . . Ama, Nathanaeli alisema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Wewe ni M—Mfalme wa Israeli." Mnaona? Ama ungekuwa ni wale wakisema ilikuwa ni Beelizebuli. Unaona mahali walipo usiku wa leo? Nashangaa mahali Nathanaeli alipo usiku wa leo. Asiyepatikana na mauti. Mnaona? Fanya chaguo lako. Hiyo ni juu yako. Unaona?

321 Lakini sasa, ninasema hilo, nikingojea kuona kama Yeye atanipa upako. Asiponipa upako, basi kuna jambo moja tu ninaloweza kufanya, enyi marafiki, ni kuomba msamaha, kwamba Yeye hajakutana nami usiku wa leo. Ndipo basi

tutaweka tu mikono juu ya wagonjwa hawa na kuwaombea, na kuwaombea baraka, tufanye wito wa madhabahuni, kisha twende nyumbani. Hivyo tu ndivyo tunavyoweza kufanya. Hivyo tu ndivyo ninavyojua kufanya.

322 Ila kama Yeye akija, basi nafikiri kila mmoja wenu aliyeinua mkono wake, kwamba ulitaka kumwona Kristo, nafikiri ni jukumu lako, mara tu hili litakapomalizika, kuja moja kwa moja hapa na kupiga magoti, na kusema, "Bwana Yesu, sasa ninajitolea Kwako."

323 Kwa sababu, kama mimi ni mwongo, Yeye kamwe hatamthibitisha mwongo. Yeye hatakuwa na uhusiano wowote na dhambi. Mungu hatakuwa nao. Bali ikiwa nimewaambia Ukweli, basi Yeye anawajibika kwa Neno Lake, ku—ku—kuthibitisha kwamba ni Kweli.

Mungu, tujalie hayo.

324 Sasa iweni tu na kicho. Mnaona? Kila mahali katika kusanyiko, iweni tu na kicho.

325 Huenda ikanilazimu kuzungumza nawe kwa dakika moja tu, mama, kitu kingine tu. Siuhisi upako juu yangu. Wala si—sikujui, na kwa hiyo hivyo ndivyo. Sasa, jambo pekee ninalotaka ufanye, kama nikikuuliza chochote, sema tu "ndiyo" ama "la." Unaona? Sasa, sababu ya mimi kufanya jambo hili . . . Hebu tuchukue tu kitu fulani, kusudi iweze . . .

326 Kamwe hatutaki kuyaacha Maandiko. Tukidumu moja kwa moja kwenye Maandiko, ndipo tunajua tuko sahihi.

327 Sasa, kwa mfano, Yesu, sasa, Yeye alikuwa huko chini katika nchi nyingine. Na Yeye alikuwa njiani Mwake kwenda Yeriko, ambayo ilikuwa moja kwa moja chini ya mlima. Lakini alikuwa na haja ya kupitia Samaria, juu *huku*. Sasa, Baba alikuwa amemtuma huko juu. Yesu alisema . . .

328 Katika mlango unaofuata, mlango wa 5, wakati alipomponya mtu aliyekuwa na tatizo fulani. Maelfu ya watu walikuwa wamelala pale, umati wa vilema, vipofu, viwete, waliopooza, wakingojea kutibuliwa kwa maji. Naye Yesu akapitia pale, Naye akamwona mtu aliyekuwa na ugonjwa uliodumaa, labda TB, au shida ya kibofu dume, ama kitu fulani. Naye akamponya, kwa sababu Yeye alijua alikuwa pale, na alijua alikuwa hivyo. Akaenda zake, akauacha huo umati mwingine pale. Akaenda zake, akaondoka. Tunajua hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli?

329 Wakapata, Wayahudi wakampata, wakamwuliza swali. Wangemwuliza Yeye swali tena usiku wa leo. "Mbona Yeye akafanya hivyo? Kama Yeye yuna huruma, na anampenda kila mtu, ni kwa nini Yeye akauacha umati huo wote wa walemavu, vipofu, viwete, waliopooza wamelala pale?"

330 Alimponya mtu mmoja tu ambaye hakuwa mgonjwa sana. Haukuwa umwue. Alikuwa nao, miaka thelathini na

minane. Ulikuwa umedumaa. Angeweza kutembea. Kasema, "Ninaposhuka kwenye birika, mtu mwingine hunitangulia huko." Mnaona? "Mtu mwingine huenda mbele yangu." Lakini Yeye akamfanya mtu huyo mmoja mzima.

331 Basi Yeye alipoulizwa swali, haya hapa Maneno Yake. Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe; ila lile ambalo Yeye amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile."

Kwa hiyo wakati alipopanda kwenda Samaria, Bwana alimwongoza kule juu.

332 Sasa, Bwana aliniongoza, mtumishi Wake, kuja Phoenix. Aliniongoza huku usiku wa leo. Sasa mimi huyu hapa, nikitoa madai Yake.

333 Sasa, wakati Yesu alipopanda kwenda Samaria, kitu cha kwanza alichokutana nacho kilikuwa ni mwanamke aliyekuja mbele Zake. Alizungumza naye mpaka akapata hali yake. Wakati alipomwambia, upesi alitambua kwamba ama ni nabii au Masihi aliyeahidiwa. Yeye alisema alikuwa ni Masihi. Mnaona?

334 Kwa hiyo tunajua manabii walikuwa katika siku zilizopita. Siku hizi ni Kristo. "Mungu zamani za kale na kwa njia mbalimbali alisema na baba zetu kwa nabii; katika siku hizi za mwisho kupitia Mwana Wake, Kristo Yesu," ambaye ni Roho Mtakatifu ndani yetu.

Sasa Yeye yupo hapa.

335 Unatambua jambo hilo. [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ninataka kukuuliza, kama Mkristo mmoja kwa mwingine. Mara tu nilipoangalia kule, ungeweza kujua jambo fulani lilikuwa limetukia, Roho mtamu sana, mnyenyekevu. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli, kusudi watu wapate kuona. Mnaona? Sasa, sasa hivi, mkimwangalia huyu mwanamke, kama mnaweza kumwona (Mnaona pale?), Nuru ya kaharabu, ikimzunguka tu huyu mwanamke.

336 Sasa yeye anaondoka kwangu. La. Ni kwa mtu mwingine. Ni mwanamke mwingine. Ni, unamwombea mwanamke fulani, mtu mwingine. Ni mama mkwe wako. Naye ana u—ugonjwa wa figo. Na—naye ana figo moja tu. Nawe unahofia kwamba ni kansa. Na hiyo ndiyo sababu wewe upo hapa, kuniuliza nimwombee. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini? Nenda, amini kwa moyo wako wote, nao haitawabidi kuiondoa. Usitie shaka. Chukua kitu hicho kidogo ulicho nacho mkononi mwako, ukiweke juu yake.

337 Unaamini kwa moyo wako wote?

338 U hali gani? Hatufahamiani, pia, sisi kwa sisi. Mara yetu ya kwanza kukutana. Na endapo . . . Mungu, kupitia kwa Mwana Wake, Yesu Kristo, amemtuma Roho Wake. Yesu alisema, "Walipo wawili au watatu wamekusanyika katika Jina Langu,

nitakuwa miongoni mwao." Hiyo ni ahadi Yake, sivyo? Sasa, Yeye hawezi kuighairi ahadi Yake.

339 Jambo pekee, ni kwamba, sisi ni hafifu sana kwa imani, hata tunakosa kumwona Yeye. Hiyo ndiyo sababu Mungu huwatuma manabii duniani. Mnaona, watu hawatasoma Biblia yao, na wao—wao hawasomi, wanaenda tu, kwa hiyo Mungu daima huwatumia ishara. Na kwa kawaida nabii ni ishara. Mnaona? Basi leo hii Roho Mtakatifu ndiye Ishara yetu, maana Yeye ni Nabii wa Mungu akitenda kazi kupitia sisi. Yeye ni Nabii wa Mungu, Ishara ya siku za mwisho.

340 Sasa, bila kukujua wewe, na pasipo kujua lolote kukuhusu. Lakini ikiwa Bwana Yesu Kristo, ambaye ndiyo kwanza niseme, kutoka kwenye Biblia, angenena kupitia kwangu na kuniambia sababu ya wewe kusimama hapo, lingekufanya uamini? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Je, ingewafanya wasikilizaji kuamini?

Sasa, Baba anasikiliza. Ninajua.

341 Unaugua ugonjwa wa wasiwasi. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

342 Sasa, mtu fulani huko nje alifikiri nilibahatisha jambo hilo. Sasa, huwezi kulificha sasa, ndugu. Linaingia hapa ndani. Mnaona? Nililipata hilo. Kamwe msiamini hilo. Kamwe msiliamini hilo. Hiyo ni dhambi. Hiyo ni kutokuamini. Mungu atawahukumu kwa sababu ya hilo. Mtawajibika kwenye Siku ya Hukumu. Ninapaswa kumwita huyo, bali kwa kawaida mimi huingia matatani.

343 Sijui kile Yeye alichokwambia. Hebu kidogo. Naam, hicho hapo, kivuli. Ni wasiwasi, unyonge. Unakudhoofisha, kufadhaika sana, umekuwa nao kwa muda mrefu. Hiyo ni kweli. Una matatizo zaidi, pia. Unaye mtu unayemwombea. Mume wako, hospitalini, anaumwa na tumbo, ndio kwanza afanyiwe upasuaji. Bibi Good, nenda nyumbani, amini kwa moyo wako wote. Na uweke hiyo juu yake, naye ata—atakuwa mzima. Mungu akubariki.

344 Hivi Yeye anakujua? Unaona? Hakika, Yeye anakujua. Sawa. Hiyo ni . . . Hivi hamtambui ya kwamba Yesu yeye yule aliyetembea katika Galilaya ni Yesu yule yule aliye hapa usiku wa leo? Hivi hamwezi kutambua jambo hilo?

345 Sasa, sijui chochote juu ya . . . Nafikiri huyo ndiye mwanamke aliyeombewa, *pale* tu. Hiyo ni kweli? Kuna yeyote wenu aliyepata kumjua mwanamke huyo? Yupo mtu anayemjua mwanamke huyo? Inua mkono wako. Mambo hayo yalikuwa sahihi? Pungeni mikono yenu, kama ndivyo. Pale *pale*. Hilo ni sawa.

346 Njoo. Wazungumza Kiingereza? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Hilo ni sawa. Mhindi? ["Mhindi."]

Ninawaheshimu ninyi; Mmarekani halisi. Sidhani. . . Mimi, kama mtu mmoja tu, siwezi kufanya uamuzi. Ninaweza tu kufanya uamuzi wangu mmoja. Nadhani hampati mgawo mzuri. Mnajua sidhani. Nafikiri, badala ya kutuma mamilioni na mabilioni ya dola, nchi za ng'ambo, wanapaswa kuwashughulikia ninyi watu. Kweli. Kweli. Kweli kabisa. Moyo wangu daima uliwahurumia. Nilikuwa huko kwenye uhifadhi wa San Carlos, si muda mrefu uliopita. Jinsi Roho Mtakatifu alivyotenda kazi mle ndani, akawaponya hao watu maskini!

347 Hatufahamiani, bwana. Sikujui. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Hatufahamiani kabisa. Hiyo ni kweli. Sisi ni mataifa mawili. Mimi ni Muanglo-Saksoni; wewe Mhindi. Ninayo damu hiyo kidogo ndani yangu kutoka kwa mama yangu. Nyanya yangu alikuwa Mcherokee. Ninaijivunia. Kweli. Lakini kama ndugu yangu, singefanya lolote kukudhuru. Ningekusaidia tu.

348 Kabila la Kihindi, lilikuwa, kama walikuwa na mmoja miongoni mwao, ambaye angeweza kutabiri na kuonyesha mahali mawindo yalipokuwa, alifanywa nabii miongoni mwao. Nao walikuwa. . . Lakini kama alitabiri jambo fulani lisilokuwa sahihi, ilibidi afe kwa ajili yake. Anapaswa kufa. Hiyo ni kweli. Hawakuwa na kutelezateleza.

349 Kama Mungu ni Mungu. . . Huenda hili taifa limewapa mgawo mbaya, bali Mungu kamwe hatawapa mbaya. Yeye alimtuma Mwana Wake kwa ajili yenu.

350 Ndio kwanza nione kile kilichotukia. Ndio kwanza utoke hospitalini. Aa-ha. Umekuja hapa upate kuombewa. Una ugonjwa wa tumbo, na umepangiwa upasuaji. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Njoo hapa.

Baba wa Mbinguni, ninaulaani ugonjwa huu wa tumbo.

351 Shetani, umejificha kutoka kwa daktari, bali kamwe hutajificha kutoka kwa Mungu. Toka kwake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Usifadhaike juu ya jambo hilo. Nenda zako, upate afya.

Mnaamini?

U hali gani?

352 Maskini mama huyu anayeketi papa *hapa,* akiomba, nyuma tu ya msichana huyu anayeketi mbele, akiwa na ugonjwa wa kibofu, unaamini Bwana Yesu atakuponya, ewe mama? [Dada huyo anasema, "Ninaamini aliniponya."—Mh.] Hiyo ni kweli.

353 Niambieni alimgusa Nani. Yeye yuko futi ishirini kutoka kwangu. Alimgusa Kuhani Mkuu, hiyo ni kweli, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Je, hamwamini jambo hilo?

354 Unaamini, mama? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? ["Ndiyo, ninaamini."] Wewe siye uliye na shida, ni dada yako. Ana kansa. Hiyo ni kweli. Usininii. . .Amini, usitie shaka. Chukua leso hiyo uliyo nayo kwa ajili yake, na uiweke juu yake. Amini kwa moyo wako wote. Atapona hiyo, ikiwa utaamini kwa moyo wako wote. Shuka uende zako. Aa-ha.

355 Iweni na imani. Unaliamini kwa moyo wako wote?

Imeondoka jukwaani. Iko kwenye kusanyiko.

356 Ni maskini mwanamke aliyekonda, anayeketi kule nyuma, aliye na TB. Ameketi kule nyuma, akiomba. Unaamini Mungu atakuponya? Unaamini? Maskini huyo mwanamke anayeangalia mbele moja kwa moja, huko nyuma kabisa. Inua mkono wako, huko nyuma, mama, papo hapo nyuma ya mwanamume huyo anayegeuka. Amini kwa moyo wako wote. Naam. Mwanamke mdogo, aliyekata nywele. Vema. Jambo ndilo hilo. Liamini, nao umekwisha.

357 Aligusa nini, huko nyuma kabisa? Ninawapa changamoto muamini.

358 Vipi kukuhusu wewe, mama? Unaamini ugonjwa huo wa mgongo ulikuacha, tangu umekuwa ukisimama hapa? Vema, basi, endelea tu. Hilo tu ndilo unalopaswa kufanya. Amini kwa yote yaliyo ndani yako.

359 Ulikuwa na jambo lile lile. Kwa hiyo kama ukiamini tu, endelea tu kupiga hatua, ukisema, "Asante, Bwana. Nipe afya." Amini kwa moyo wako wote.

360 Unahofia utakuwa kiwete kwa baridi yabisi. Sivyo? Kwa hiyo kama unaamini, amini kwa moyo wako wote, nenda ukaamini kwa moyo wako wote, upate kupona. Hayo tu ndiyo yanayokubidi kufanya, ni kuamini.

361 Mnaamini? Vipi kuhusu baadhi yenu enyi watu huko nje? Hivi mko katika imani, mnaamini?

362 Vipi kama nilikwambia Yesu alikuponya, unayesimama hapo, ungeamini? [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Anza tu kutembea, unaona, ukiamini kwa moyo wako wote.

363 Unataka kwenda nyumbani, kula chakula chako cha jioni? Unaamini maskini tumbo hilo lenye wasiwasi limekuacha? Nenda zako, ule kama unataka. Amini.

Je, mnaamini?

364 Vipi kuhusu mwanamke huyo anayeketi hapo, akimwombea maskini yule, mtoto yule, aliye na ugonjwa wa damu? Unaamini Mungu atamponya huyo mtoto? Vema, unaweza kulipokea.

365 Hilo lilimgusa mama huyo, papo—papo hapo karibu nawe hapo. Ameketi hapo akiomba kwa ajili ya ugonjwa wa wasiwasi, hiyo ni kweli, karibu na wewe. Pia, unaye ndugu aliye na

ugonjwa wa akili. Hiyo ni kweli. Unaye mama aliye na jicho baya. Kama unaamini kwa moyo wako wote, Mungu atawaponya. Amina.

366 Mnamwamini Yeye?

367 Vipi kuhusu wewe hapa, katika kiti cha magurudumu? Unaamini? Huyo ni mwanao anayeketi hapo, ambaye ndio kwanza aseme hilo wakati huo. Huyo ni mwanao. Una kansa usoni mwako. Husikii vizuri. Unatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote! Unaamini hilo kwa ajili yake, mwanangu? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Mwambie masikioni mwake. Weka mkono wako juu yake, na hebu aupokee ubatizo wa Roho Mtakatifu.

368 Mnaamini Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele?

369 Mnamwamini Masihi, yule Masihi mkuu wa Mungu, anatenda kazi miongoni mwa watu Wake?

370 Mko tayari kuacha yote na kumfuata Yeye? Ikiwa mko tayari, mwinulieni mikono yenu, na kusema, "Nitamfuata. Nitamfuata. Nitamwamini. Kila Neno analosema, nitamwamini. Nitayanyosha maisha yangu. Nitamfanyia Yeye kazi." Mungu uturehemu! Mungu awabariki.

371 Ni waaminio wangapi walio hapa ndani sasa? Inua mkono wako.

372 Ni wangapi wanaotaka kuwa karibu na Yeye? Inua mkono wako. Wote wanaotaka kuwa karibu na Yeye na kumkubali Yeye sasa hivi, Yeye yupo papa hapa. Huu ni Uwepo Wake.

373 Mwanamume yule huko nyuma mwenye ugonjwa wa tezi dume, umekwisha, ndugu. Mungu alikuponya wakati uo huo.

374 Mbona, Hiyo inaenda tu kila mahali namna hiyo, katika Nuru, ikizungukazunguka kote jengoni. Lolote laweza kutendeka sasa hivi. Tunaweza kuwa na pentekoste nyingine, kama tu mkiamini.

375 Simama kwa miguu yako, kila mmoja wenu. Mwinulieni Mungu mikono yenu. Mpeni sifa.

376 Asante, Bwana Yesu. Tunakuabudu Wewe, Baba, kwa sababu kwamba Wewe ni Mwokozi wetu na Mungu wetu. Upo hapa. Umelithibitisha Neno. Umelithibitisha kuwa hivyo. Wewe ni Mungu, Masihi, yeye yule jana, leo, na hata milele. Pasipo kushindwa, pasipo na shaka, Wewe ni Bwana Yesu yeye yule. Jina Lake Takatifu na lisifiwe!

377 Mnampenda? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

378 Ni wangapi wenu walio waaminio sasa? Inua mkono wako. Sasa, Yesu alisema hivi, Mwenyewe, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Mimi siye tu niliye na Roho Mtakatifu. Mnaye,

pia. Wewe ni mwaminio, sawa tu na mimi nilivyo mwaminio. Sasa yaache mashaka yako yote.

379 Weka mkono wako juu ya mtu fulani na kuamini ya kwamba Mungu atamponya mtu huyo, kulingana na Neno Lake. Kama Yeye atatimiza la namna hii. . . Weka mkono wako juu ya mtu fulani, anza kuwaombea, useme, "Bwana, mponye mtu huyo." Omba uone linalotukia. Wewe ni mwaminio.

380 Mwenyezi Mungu, katika Jina la Yesu Kristo tulimshinda ibilisi. Tumemkemea, na kuzirarulia mbali nguvu zake kutoka kwake. Kwa kupigwa kwa Bwana Yesu Kristo tunaponywa.

Kuacha Yote SWA62-0123
(Forsaking All)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumanne jioni, tarehe 23 Januari, 1962, kwenye Sunnyslope Assembly Of God huko Tempe, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org